# Nipashe

Jumanne Septemba 22, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580346

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

CWT jiongezeni, wanachama wanahitaji kujua ujasiriamali

NA CHRISTINA MWAKANGALE

MZAZI INAKUHUSU

- Mama ukijifungua ndani ya saa moja uwe umenyonyesha
- Mgusishe mtoto chuchu hata kama hazitoi maziwa

UKURASA 11



## Serikali yawatangazia kibano waganga wa jadi, tiba mbadala

UKURASA 4

# Magufuli: Vitambulisho wamachinga sio lazima



UKURASA 2

## Mgombea aliyekatwa, kurejeshwa afunguka

UKURASA 3


Lissu


Lipumba


Maalim

## Lissu, Maalim Seif, CUF wakoleza moto kampeni

UKURASA 2,3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# CUF yajitapa kuweka kwa vijana

**Na Boniface Gideon,** KIGOMA

MGOMBEA mwenza wa urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Hamida Abdallah Huweish, amesema iwapo chama hicho kitapata ridhaa ya kuingia madarakani, serikali yake itawekeza kwa vijana kwa kuwapatia ajira na kunufaika na rasilimali za nchini katika kujenga uchumi wa watu na siyo vitu.

Huweish aliyasema hayo wakati akiomba kura za rais, wabunge na madiwani katika Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Alisema viongozi wengi wamesahau kuwekeza kwa vijana ambao ndio waathirika wakubwa wa kukosa ajira na badala yake wamewekeza kwenye ununuzi wa uchumi wa vitu badala ya uchumi wa watu.

"Serikali ya CUF itarudisha uchumi kwa wananchi na tutawekeza kwa vijana zaidi ambao wengi wao ni waathirika wa kukosa ajira, lakini mtamiliki uchumi wenu na sio serikali imiliki uchumi na kupelekea ugumu wa maisha," alisema Hamida.

Alisema jambo kubwa la serikali ya CUF itakuwa ni kurudisha mzunguko wa fedha kwa wananchi na kutengeneza mazingira rafiki kwa wafanyabiashara ambayo yatawarahisishia katika mzunguko wao wa fedha ikiwamo kutengeneza miundombinu mizuri ya masoko, kodi za bidhaa zao na barabara za vijijini.

"Wananchi wa Kigoma najua wengi wenu ni wakulima, ipo adha mnayoipata niwahakikishie sera ya CUF ni kuboresha miundombinu, kapigeni kura ili tufanye mabadiliko na kubadilisha uchumi wenu," alisema.

Akizungumzia nyongeza za mishahara ya wafanyakazi, Hamida alisema ikiwa chama hicho kitapata ridhaa kitahakikisha kinabadilisha maisha ya wafanyakazi ikiwamo kupandisha mishahara.

Kuhusu matibabu kwa wazee, alisema sera ya chama hicho ni kuhakikisha mzee kuanzia miaka 60 anakuwa na kitambulisho maalum kwa ajili ya kutibiwa bure.

"Endapo tukipata ridhaa ya kuongoza nchi elimu ya msingi na sekondari itakuwa bure, lakini kwenye suala la afya tutahakikisha huduma kwa mama mjamzito hadi mtoto atakapofikisha miaka miwili inakuwa bure," alisema.

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya, alisema sera ya chama hicho endapo kitapata ridhaa ni kuhakikisha wazee kuanzia miaka 60 wanakuwa na vitambilisho maalum kwa ajili ya kupata matibabu.

Alisema hali ya uchumi imekuwa ngumu hasa kwa wafanyabiashara wadogo kutokana na kutozwa fedha kwa ajili ya kitambulisho.

"Ukishindwa kupanga mmechagua kufeli, wapo wafanyabiashara mtaji wao haufiki hata elfu kumi, lakini unamwambia atoe elfu ishirini kwa ajili ya kitambulisho huu ni unyonyaji," alisema Sakaya.

Aliongeza: "Wanatangaza viwanda, lakini hakuna ajira, na kuwa ajira itapatikana katika ilani ya CUF kwa sababu ilani yake ni kuboresha maisha ya Mtanzania ambayo yatamfanya kuendesha maisha yake."

Mgombea ubunge Jimbo la Kigoma Kusini, Gerald Serikali, akiomba kura alisema akipata ridhaa ndani ya kipindi cha miezi kumi atasimamia ujenzi wa bweni la wasichana Shule ya Sekondari Nguruka.

Alisema pamoja na ujenzi wa bweni atahakikisha anasimamia ujenzi wa Zahanati ya Lugongoni 'A' kwa kushirikiana na wananchi pamoja na fedha za mfuko wa jimbo.

# JPM: Vitambulisho vya wamachinga si lazima

**Na Gwamaka Alipipi, TABORA**

RAIS John Magufuli amewakemea baadhi ya wakuu wa wilaya wanaowalazimisha wafanyabiashara wadogo kununua vitambulisho, kwa kuwaeleza kuwa ni hiari kwa mfanyabiashara kuwa nacho au la.

Amesema serikali ilianzisha mchakato wa kuuza vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kuwasaidia kutosumbuliwa na askari mgambo wa jiji, pindi wanapouza bidhaa zao mitaani.

Alitoa kauli hiyo jana mkoani Tabora, wakati akizungumza na maelfu ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi waliojitokeza katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, kumsikiliza akimwaga sera na kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kwa awamu ya pili kuwa rais.

"Vitambulisho havilazimishwi, elimu itolewe kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kuwa na vitambulisho hivyo. Tunatoa vitambulisho ili wafanyabiashara wasisumbuliwe, vitambulisho havitolewi kwa bunduki bali vinatolewa kwa Sh. 20,000," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"DC (Mkuu wa Wilaya) wa hapa azingatie maelekezo haya. Kama kuna mfanyabiashara ambaye hataki kitambulisho aende kwa mgambo akamwagiwe chakula chake, anyang'anywe bidhaa zake. Ndiyo maana tukasema walipe kiasi hicho, ndiyo faida utafanya biashara popote, hayo ndiyo maagizo yangu."

**KUINUA ZAO LA TUMBAKU**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli aliwahakikishia wakulima wa zao la tumbaku wa mkoa huo, kuwa changamoto zinazowakabili ikiwamo kukosa wanunuzi, bei ndogo, kuchelewa kwa malipo zitatatuliwa.

Alisema katika kutatua changamoto hizo ndiyo sababu alimteua Hussein Bashe kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, kutoka mkoa huo.

"Najua kuna changamoto hapa ya soko la tumbaku, limekuwa tatizo sugu kwa mkoa huu, watu wanalima wanakosa wanunuzi, bei inakuwa ndogo, malipo yanachelewa, wekeni imani kwangu tutalibeba kwa nguvu zote, mnafahamu nilimteua Bashe afuatilie ili tujue chanzo cha tatizo," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alibainisha kuwa bei ya masoko mengi ya mazao kama tumbaku, pamba, korosho ilishuka kwa sababu ya mlipuko wa ugonjwa wa corona, hali hiyo ilisababisha wazungu ambao ni wanunuzi kujifungia ndani, ndege, meli zilishindwa kusafiri.

Rais Magufuli alisema: "Sasa utapeleka wapi wakati wanunuzi wamejifungia? Mnaojua sababu za msingi mnasema serikali haitaki kununua tumbaku, walipaswa waseme ukweli kuwa mambo yamevurugika kule maana corona ilikuwa utumwa wa kishetani na wa ajabu."

**AKEMEA UBAGUZI**

Aidha, Rais Magufuli alikemea baadhi ya wanasiasa wanaotoa sera za kibaguzi, kuwagawa Watanzania.

Alisema sera za kuligawa Taifa ni mbaya na inapaswa kukemewa vikali na Watanzania, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliyaunganisha makabila ya Watanzania zaidi ya 121, kuwa kitu kimoja.

"Kuna watu nawasikia wanasema wakipewa nchi eti wataanzisha serikali za majimbo, yaani kila mkoa uwe na utawala wake, nawaomba Watanzania tusigawanywe kwa ukabila, udini wala ukanda, sisi ni ndugu," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Tabora mngekuwa na jimbo lenu, ukishagawanywa ni mwanzo wa mfarakano kwa sababu kila jimbo litakuwa linajitegemea lenyewe. Likiwa maskini litakuwa maskini wa kutupwa. Nyerere alipokuwa akiomba uhuru wa Taifa hili, angeamua kuligawa kwenye majimbo tusingefika hapa," alisema Rais Magufuli.

**KUIJENGA TABORA**

Kadhalika, Rais Magufuli aliwahakikishia wananchi wa Tabora kuwa na miundombinu ya kisasa, upatikanaji wa umeme na uhakika pamoja na maji.

Rais Magufuli alisema: "Tumetenga Sh. bilioni 567 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami kilometa zaidi ya 300 katika mkoa wa Tabora, tumeupanua uwanja wa ndege na sasa tunajenga jengo la abiria pamoja na njia ya kuruka ndege tunazidi kuipanua, tunataka ndege kubwa zilete watalii."

Aliongeza: "Tumeanzisha hifadhi za wanyama Kigosi, Mto Ugala, lengo kuu ni kuwavutia watalii kuja Tabora. Mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria utafika Tabora mjini utaenda hadi Urambo, nataka wananchi waoge maji."

**MAFANIKIO MIAKA MITANO**

Rais Magufuli alisema serikali imefanikiwa kuimarisha miundombinu ya usafiri na huduma ya maji katika mkoa wa Tabora.

Alisema Sh. bilioni 600 zimetumika katika kutoa maji katika Ziwa Victoria hadi mji wa Nzega-Tabora Mjini-Igunga, kwamba asilimia 92 ya ujenzi wa mradi huo umeshakamilika.

Alisema miradi ya maji 50 imetekelezwa katika mkoa huo kwa gharama ya Sh. bilioni 11.5 ikiwamo vijiji vya Igombe, Kaliua.

Kuhusu barabara, Rais Magufuli alisema kupitia mradi wa kuendeleza miundombinu kwenye miji nane, mkoa wa Tabora umefanikiwa kujengwa barabara za lami pamoja na taa.

Alisema: "Zamani barabara ya Tabora-Itigi-Manyoni- ilikuwa vumbi, Tabora Nzega ilikuwa vumbi, sasa hivi ni lami. Sasa hivi tunataka kujenga barabara ya lami hadi Nyakanazi-Kigoma, mkandarasi yuko eneo la kazi."

Kabla ya mkutano wa mjini Tabora jana, Rais Magufuli alihutubia mikutano kadhaa ya kampeni mkoani humo.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wanachama wa chama hicho na wananchi wa kijiji cha Makoga Jimbo la Wanging'ombe, alipokuwa njiani akielekea wilayani Makete, mkoani Njombe jana, kwa ajili ya kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: OMR.**

# Maalim Seif ajinadi kuuboresha utalii

**Na Rahma Suleiman,**

**ZANZIBAR**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema kuwa endapo atapata ridhaa za wananchi ataimarisha sekta ya utalii.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kampeni uliofanyika viwanja vya Mwanakombo Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati akinadi sera zake.

Alisema ataifanya sekta hiyo kuwa ni chanzo cha kukuza uchumi kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Alieleza kuwa kuna vikwazo mbalimbali vya utalii Zanzibar, hivyo akiwa rais ataandaa nembo maalum ya Zanzibar katika utalii akitolea mfano kwa India.

"Sisi tumebahatika kuwa tuna jina zuri ambalo huvutia wageni, lazima ukubali kuwekeza na ugharamike.

Kama huwekezi na ukashiriki na ukaipeleka Zanzibar katika macho ya watu duniani, utaalii utabaki chini," alisema Maalim Seif.

Aidha, alisema atahakikisha anatoa mafunzo ya kilimo na ufugaji kwa vijana ili wajiajiri na kuondokana na changamoto ya ajira.

Alieleza kuwa atakifanya kilimo kiwe na tija zaidi ili vijana kujiajiri karika sekta hiyo na kupata kipato.

Alisema kilimo kitaimarishwa ili wananchi wasilalamike kuwa wana njaa na maisha yao yatakuwa mazuri.

"Pia tutahakikisha tunakuwa na soko zuri ili wakulima wetu waweze kuuza mazao yao," alisema.

Alisema ataanzisha viwanda vya kuhifadhi mazao pamoja na vya kutengenezea juisi ya matunda mbalimbali ili wakulima wanufaike na kilimo.

Mgombea huyo pia alisema ataanzisha kilimo cha maua na kuimarisha soko la kilimo hicho ili kuuza nje ya nchi ikiwamo Dubai.

# Lissu kutoa vitambulisho vya wamachinga bure

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema akichaguliwa kushika nafasi hiyo atatoa bure vitambulisho vya wajasiriamali.

Lissu alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia wananchi wa Ngara mkoani Kagera.

"Kwenye uchaguzi mkuu huu tunahitaji kufanya mabadiliko makubwa sana, mojawapo ya mabadiliko hayo ni pamoja na kuondoa manyanyaso ikiwamo ya wananchi kuuziwa vitambulisho vya wajasiriamali," alisema Lissu.

"Kwa nini muuziwe vitambulisho, nchi hii vitambulisho vinatolewa bure lakini kwa sasa vinauzwa, hayo yote mwisho ni Oktoba 28, mwaka huu, mkituchagua."

Pia Lissu alisema serikali yake itasaidia watu wenye shida hususani wanapokumbwa na balaa ikiwamo, mafuriko, njaa na majanga mengine ya kibinadamu.

"Mojawapo ya kazi ya rais ni kusaidia watu wenye shida na imetungiwa sheria. Kuna sheria ambayo imetungwa na bunge ambayo imewekewa utaratibu wa namna ya kusaidia watu panapotokea balaa au mafuriko, tetemeko la ardhi, mafuriko, njaa au matatizo mengine," alisema Lissu.

"Kazi nyingine ambayo serikali inaweza kufanya katika kipindi cha majanga kama hayo ni kununua chakula ambacho wananchi watanunua kwa bei rahisi wanapokutwa na majanga."

Mgombea huyo wa urais wa CHADEMA, jana, alifanya mikutano katika maeneo mbalimbali ikiwamo Ngara na Nyakanazi ambako alisimamishwa na wananchi wakati akielekea katika mikoa ya Kagera na Geita kuendelea na kampeni zake za kunadi sera za chama chake na kuomba kura.



Mgombea mwenza wa urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Hamida Abdalah Huweish, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu wilayani Uvinza, mkoani Kigoma jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Mgombea aliyeenguliwa na kurejeshwa afunguka

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Morogoro Mjini kupitia CHADEMA, Devotha Minja, aliyakuwa ameenguliwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo hilo na baadaye kurejeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), amefunguka kwa kuiomba tume kumwondoa msimamizi huyo kwa madai ya kuonyesha upendeleo mapema.

Akizungumza na Nipashe, alisema sababu zilizoeleza kuhusu kuenguliwa kwake ni kudaiwa kuwa fomu zilizobandikwa hazikuwa na picha zake na kwamba alikuwa na nakala ambazo zilikuwa na picha, baada ya kukata rufani zilionekana.

"Naishukuru NEC ila sina imani na msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo la Morogoro Mjini, kama ameweza kuondoa picha zangu maana yake hata nikishinda hatanitangaza, ninaomba NEC imwondoe tupewe msimamizi mwingine," alisema Minja.

Aidha, alisema kwa sasa ameanza kampeni za nyumba kwa nyumba kuhakikisha anawafikia wananchi wengi zaidi, na kwamba jana alikuwa katika Kata ya Lukobe na anatarajia kufanya kampeni katika kata za Kihonda na kwingineko.

Minja ambaye alikuwa mgombea wa viti maalum mkoani Morogoro kwa miaka mitano, alisema vipaumbele vyake vitakuwa ni kuhakikisha Morogoro ina hospitali ya wilaya tofauti na hali ilivyo sasa kuna hospitali ya mkoa ambayo ni ya rufani.

Alisema kipaumbele kingine ni kuboresha huduma za maji na kwamba mji huo kuna mito 52 inayotiririsha maji, lakini wananchi hawana maji nyumbani.

Pia atahakikisha viwanda vyote vilivyokufa vinafufuliwa ili kufanya wanawake wengi wapate ajira.

Akiwa kwenye mkutano wa kampeni jana, alisema kuwa mkoa huo umebarikiwa kuwa na viwanda vingi, lakini havifanyi kazi kwa kuwa vilichukuliwa na watu wasiokuwa na uwezo wa kuviendesha.

"Mkoa wa Morogoro hususani Manispaa ya Morogoro kuna viwanda vingi ambavyo havizalishi, nikichaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hili nitajitoa kuhakikisha viwanda hivyo vinafanya kazi ili kinamama wa Morogoro wapate ajira katika viwanda hivyo," alisema Minja.

Pia alisema viwanda ni mkombozi wa ajira kwa wanawake kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa hupata ajira kwa wingi viwandani kuliko ofisini na hivyo kuwawezesha kujikimu katika maisha yao ya kila siku.

"Mfano kiwanda cha tumbaku ambacho kwa sasa kimesimama uzalishaji kilikuwa kinaajiri watu 5,000, wengi wao wakiwa wanawake, ambao wanaweza wakapata hata kazi ya kupepeta, kufanya usafi, kufunga na mengineyo ni viwandani," alisisitiza.

Kadhalika, alisema maisha ya wakazi wa Morogoro yamekuwa magumu kwa kuwa wengi wao hawana ajira kutokana na viwanda vingi kufungwa.

"Mimi nitakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba tunafufua hivyo viwanda, kwa sababu vilijengwa kwa jasho na kodi za Watanzania, vilibinafsishwa vikiwa vinafanya kazi, lakini waliovimaliza na kuviua viwanda hivyo lazima tupambane nao, kama walishindwa kuviendeleza walitakiwa kuvirudisha serikalini," alisema.

Aliyekuwa mfanyakazi wa kiwanda cha tumbaku, Zaituni Hussen, alisema athari ni kubwa katika maisha yao kutokana na kukosa ajira baada ya kiwanda hicho kufungwa na kuwafanya kutetereka kimaisha, huku wakiomba Mungu kila siku serikali ifungue kiwanda hicho.

# Serikali yatoa angalizo waganga jadi

**Na Happy Severine,** ITILIMA

SERIKALI imewatahadharisha waganga wa tiba asilia na mbadala kuacha kutumia nyara za serikali katika shughuli zao zikiwamo ngozi za wanyama wa porini kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa.

Tahadhari hiyo imetolewa jana Wilaya ya Itilima, mkoani Simiyu na Ofisa Maliasili wa wilaya hiyo, Goodluck Malisa, alipozungumza na waganga hao.

Alisema kumiliki na kubeba nyaraka hizo bila kibali maalum ni kosa na ni kinyume cha sheria kifungu cha 86 (1), 2 (b) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori na 5 na kifungu cha 57 (1) na 60 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Benson Kilangi, aliwataka waganga hao kufanya kazi kwa kufuata sheria ikiwamo kusajiliwa.

Aliwaambia kuwa taaluma hiyo inapaswa kuheshimiwa na kwamba njia pekee ya kuwawezesha kufanya kazi vizuri ni kufuata sheria za nchi.

Meneja Msaidizi kutoka 'Doctors with Africa' (CUAMM) Mkoa wa Simiyu, Flora Mayanda, alisema wataendelea kushirikiana na serikali ya mkoa kuhakikisha mafanikio na matokea chanya yanafikiwa.

Kwa upande wao, waganga wa tiba asili na mbadala mkoani Simiyu, wameahidi kupitia umoja wao kuchangia shughuli za maendeleo ikiwamo uchangiaji damu wenye lengo la kuokoa maisha ya wahitaji wa huduma hiyo.

Waliahidi kuendelea kujitokeza kwa wingi kujisajili, ili watambulike kisheria hatua itakayowasaidia kufanya kazi zao kihalali kwa kuzingatia kanuni na taratibu za nchi na kwamba mkoa nzima una jumla ya waganga 4,353.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika viwanja vya Shule ya Msingi Kakola, Jimbo la Msalala mkoani Shinyanga jana. **PICHA: FRANCIS DANDE**

## Kampeni Jimbo la Mpendaye kuanza leo

**Na Betrina Bishubo,** SJMC

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema kuwa kampeni za uchaguzi katika Jimbo la Mpendaye visiwani Zanzibar, zinaanza leo baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kupata jina la mgombea ubunge mwingine.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, alipokuwa akihojiwa kuhusu uchaguzi mkuu.

Mgombea wa jimbo hilo, Salimu Abdullah Turky (57), kwa jina maarafu 'Mr White' alifariki Septemba 15, mwaka huu na kufanya nafasi hiyo kuwa wazi.

Kwa mujibu wa Jaji Kaijage, uteuzi wa mgombea wa CCM umefanyika jana na vyama vyote vitaruhusiwa kuendelea na kampeni baada ya mgombea huyo kupatikana.

"Huyu aliyepoteza maisha na Tume imeshajulishwa imeshaweka ratiba ya uteuzi kwa chama kilichopoteza mgombea wake," alifafanua.

Alisema ratiba ya uchaguzi mkuu kwa jimbo hilo itabaki kama ilivyo na msimamizi wa uchaguzi ameshafuata taratibu zote za kuhakikisha kampeni zinaendelea.

Kipenga cha kampeni za uchaguzi kilipulizwa Agosti 25, mwaka huu, kwa vyama kuanza kunadi ilani na sera zao kwa ajili ya wananchi kuwachagua katika nafasi za urais, ubunge na udiwani.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC pamoja na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), uchaguzi mkuu utafanyika Jumatano ya Oktoba 28, mwaka huu.

Moja ya majukumu ya NEC kipindi cha uchaguzi ni kuvikumbusha mara kwa mara vyama vya siasa sheria na taratibu zinazotakiwa kufatwa wakati wote wa kampeni.

# Kesi ya Kubenea yapigwa kalenda

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KESI ya aliyekuwa Mbunge wa Ubungo jijini Dar es Saalam, Said Kubenea, imepigwa kalenda hadi Oktoba 19, mwaka huu, baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, kuelezwa jalada la upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Martha Mahumbuga, alilazimika kuahirisha shauri hilo baada ya Wakili wa Serikali, Innocent Njau, kuiomba mahakama hiyo kupanga tarehe nyingine.

"Mheshimiwa Hakimu, tunaomba tarehe nyingine ya kutajwa kesi hii kwa sababu bado hatujakamilisha upelelezi," alisisitiza.

Wakili wa Utetezi, Shecky Mfinanga, akisaidiana na Allute Munghwai, waliieleza mahakama hiyo kuwa katika jopo lao ameongezeka wakili William Mwisijo.

Baada ya ombi hilo, Hakimu Mahumbuga alisema kesi hiyo, itatajwa tena Oktoba 19, mwaka huu.

Septemba 7, mwaka huu, Kubenea alisomewa mashtaka yake na Wakili wa Serikali Innocent Njau, likiwamo kosa la kuingia nchini kinyume cha kifungu cha 45(1)(i) na (2) cha Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54.

Alidai kuwa mshtakiwa alikamatwa katika mpaka wa Namanga uliopo mkoa wa Arusha, Septemba 5, mwaka huu na baada ya kupekuliwa alikutwa na fedha za kigeni.

Katika shtaka la pili, anadaiwa kuingiza nchini fedha za kigeni bila kutoa tamko kinyume na kanuni ya utoaji tamko la fedha mpakani za mwaka 2016.

Kubenea aliachiwa kwa dhamana Septemba 11, mwaka huu, baada ya kulipa Sh. milioni 14.5.

# NEMC: Elimu imedhibiti magonjwa ya mlipuko

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeeleza kuwa kupungua kwa kasi ya magonjwa ya mlipuko hususani kipindupindu nchini, kumetokana na usimamiaji mzuri wa sheria na kanuni za mazingira na utoaji wa elimu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwapongeza Watanzania kwa kuweka mazingira safi na salama kwa hiari.

"Tabia ya kuchukia uchafu na kutunza mazingira ambayo imejengeka katika jamii yetu, ni jambo zuri sana. Kuheshimu sheria ya mazingira na kanuni zake kwa hiari ni kitu muhimu katika kulinda na kutunza mazingira, kulinda afya za watu na viumbe wengine," alikiambia kikundi cha watu alichokikuta kinasafisha eneo lao kwa hiari.

"NEMC katika kipindi cha miaka mitano tumetoa elimu kupitia vyombo vya habari na kuandaa mikutano mbalimbali ya wadau wa mazingira na wananchi kwa ujumla wake. Tumepata mafanikio makubwa kwani takwimu zinaonyesha magonjwa ya milipuko kama kipindupindu kasi ya kuenea kwake imepungua sana, sikumbuki kama tumekumbana na kipindupindu miaka mitano iliyopita," alisema.

Aliongeza kuwa chanzo kikubwa cha magonjwa ya milipuko nchini ni utiririshaji wa majitaka katika maeneo ya makazi ya watu pamoja na maji ya kemikali zenye sumu kutoka viwandani ambayo huelekezwa katika mito na makazi ya watu.

# NCC kufundisha mbinu bora utatuzi migogoro kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Ujenzi la Taifa (NCC), linatarajia kutoa mafunzo ya siku tatu utatuzi wa migogoro ya kibiashara jijini Dar es Salaam, kuanzia Septemba 23 kwa makundi yote ya wahandisi na wataalamu wa sekta nyingine nchini, waliothibitisha ushiriki wao.

Mtendaji Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Matiko Mturi, alisema mafunzo hayo yataendeshwa na wataalamu wabobezi wa masuala ya sheria na utatuzi wa migogoro ya kibiashara, jijini Dar es Salaam na kuhusisha wadau wote wa sekta ya ujenzi; wahandisi, wakadiriaji majengo, mameneja majengo na miradi, wasanifu majengo, wajenzi, wakaguzi wa viwango pamoja na wataalamu wa sekta nyingine mbalimbali wakiwamo wanasheria, maofisa bima na wanaotoka katika sekta ya usafirishaji majini.

Alisema washiriki waliotaka kuhudhuria mafunzo hayo kwa kipengele cha kutahiniwa pekee, yaani kufanya mitihani, wameruhusiwa kufanya hivyo kulingana na masharti na vigezo vilivyotolewa na NCC kwa kulipa ada ya Sh. 350,000 kwa mshiriki, tofauti na iliyopaswa kulipwa na wanaohudhuria mafunzo yote, ambayo ni Sh. 750,000.

Kwa mujibu wa Dk. Mtiru, lengo la mafunzo hayo ni kuandaa watatuzi bora wa migogoro ya kibiashara kwa njia mbalimbali zinazokubalika kisheria, ikiwamo usuluhishi, watakaozingatia sheria na haki watatuapo migogoro, kutokana na misingi bora watakayofundishwa.

"Baraza linaendesha mafunzo haya kwa mara ya 14 sasa na yamekuwa ya mafanikio wakati wote, kutokana na mrejesho tunaoupata kupitia watatuzi wa migogoro husika, wasuluhishwa, utafiti tunaoufanya kutafuta mrejesho na njia nyingine za kupata taarifa ikwamo kupokea maoni ya wadau," Dk. Mtiru alisema.

Akifafanua kuhusu ada, alisema ni kwa ajili ya kulipia vifaa na gharama za chakula.

Vile vile, alisema wahitimu watapewa mitihani itakayogusia mambo muhimu waliyofundishwa kulingana na miongozo ya kozi husika.

Alitaja baadhi ya maeneo yatakayofundishwa kuwa ni pamoja na jinsi ya kuandaa utatuzi wa migogoro hiyo kwa njia mbalimbali, ikiwamo usuluhishi, sheria za kufuata, namna ya kuzitekeleza kufikia muafaka kusudiwa, vipengele muhimu katika utatuzi wa migogoro hiyo, gharama, jinsi ya kumpata msuluhishi, nguvu ya msuluhishi, namna ya kumaliza mgogoro ulio mahakamani na maeneo mengine.

# Majaliwa: Agizo upunguzaji kodi sekta ya uvuvi limetekelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema Ilani ya chama hicho ya mwaka 2015 -2020 ilielekeza upunguzaji wa kodi kwenye sekta ya uvuvi, na agizo hilo limetekelezwa.

Alitoa kauli hiyo jana, wakati akizungumza na wakazi wa Kata ya Bukima, wilayani Musoma, mkoani Mara katika mkutano uliofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Majita.

Majaliwa ambaye yuko mkoani Mara kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, aliwaombea kura pia mgombea ubunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo na madiwani wengine wa wilaya hiyo.

Mgombea udiwani wa kata ya Bukima, Januari Simla alipita bila kupingwa.

"Katika kutekeleza Ilani ya CCM, tumepunguza kodi kwenye malighafi na zana za uvuvi, kwenye injini za uvuvi, nyuzi za kushonea nyavu za kuvulia samaki, vifungashio na kwenye ada za leseni za kuvulia samaki," alisema.

Akielezea mambo mengine yaliyofanyika kwenye sekta hiyo, amesema kazi kubwa iliyofanyika ni kuwatambua wavuvi na kuwaweka kwenye vikundi kazi ambayo alisema imesaidia kuongeza vikundi hivyo kutoka 37 hadi kufikia 113.

"Ni kwa nini tuliamua kuwaweka kwenye vikundi ni kwa sababu inakuwa rahisi kuwafikia, kuwaelimisha na kuwahudumia. Hii imefanikisha idadi ya samaki wanaovuliwa iongozeke kutoka 415,000 hadi 800,000."

Alisema kiwango cha uvuaji samaki kimeongezeka kutoka tani 300 na kufikia 448, 467. "Kikubwa ninachowaomba ni kwamba, tumieni vyombo vya kisasa kuvua samaki ili kutunza mazalio yao."

Akiwa njiani kuelekea Musoma Mjini, Majaliwa katika kata za Kusenyi, Mugango na Mkirira, pia aliwaombea kura wagombea wa urais, ubunge na udiwani kwa tiketi ya CCM.



Ofisa Vipimo wa Wakala wa Vipimo (WMA) mkoani Geita, Lightness Justine (kulia), akitoa elimu kuhusu mawe maalum yanayotumika kuhakiki mizani ya madini, wakati wa maonyesho ya madini yanayoendelea kwenye viwanja vya Bombambili, mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mgombea aahidi wanawake SACCOS

**Na Timothy Itembe,** SERENGETI

MGOMBEA wa ubunge wa Jimbo la Serengeti mkoani Mara, Catherine Ruge (CHADEMA), amejinadi kwa wanawake na kuahidi kuwa endapo akichaguliwa kuwa mwakilishi wa wananchi wa jimbo hilo, ataanzisha SACCOS maalum kwa ajili yao ili kuwawezesha kupata mikopo.

Akizungumza kwenye mkutano wa ndani uliowajumuisha baadhi ya wanawake Jimbo la Serengeti bila kujali itakadi zao za vyama, Ruge aliwaomba kumchagua na kuwa mbunge wao ili ahakikishe anawaletea maendeleo ikiwamo kuunda SACCOS kwa lengo la kukopa kwa riba nafuu.

"Niwaombe wanawake wenzangu mnipigie kampeni kwa wapigakura ili nikichaguliwa kuwa mbunge nitatue matatizo yenu kwa sababu nayajua ikiwamo ukosefu wa mitaji, lakini mkinichagua nitaenda kuwatetea bungeni pamoja na kuanzisha SACCOS kwa lengo la kukopa na kulipa kwa riba ya gharama nafuu," alisema Ruge.

Alisema, Jimbo la Serengeti linakabiliwa na changamoto ya majisafi na salama jambo ambalo akiingia bungeni atalipigania na kuhakikisha kuwa wanawake wanapata huduma hiyo. Mgombea huyo aliongeza kuwa sababu kubwa inayomsukuma kuanzisha SACCOS, ni kutaka kuwasaidia wanawake ambalo ni kundi linalobeba familia.

Kwa upande wake, Magreth Juma, alimwomba mgombea huyo kuwatetea na kuhakikisha anatimiza ahadi na asije akawageuka.

Magreth aliongeza kuwa wanawake na wananchi wa Serengeti kwa ujumla wanahitaji kupata uwanja wa ndege ili kuongeza mapato kutokana na watalii kuingia na kutoka mbuga ya Serengeti.

Weisiko Genya, alisema kuwa umeme wanaotumia wilayani hapo unasumbua endapo mbunge huyo atafanikiwa kuchaguliwa awasaidie kutatua tatizo hilo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba wanateketea, hatua zichukuliwe

**JANA** tulichapisha ripoti maalum iliyoonyesha jinsi simba wanavyozidi kupungua kutokana na kuuawa kwa kuwekewa sumu na wananchi katika ikolojia ya Tarangire Manyara yenye ukubwa wa kilomita za mraba 35,000.

Mtafiti wa simba katika eneo hilo, Dk. Bernard Kassui ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Masomo ya Usimamizi wa Wanyamapori cha SFS, alisema mwaka 2003 eneo hilo lilikuwa na simba zaidi ya 200, lakini kwa sasa inakadiriwa kuwa 180.

Utafiti umeonyesha idadi ya mifugo katika eneo hilo imeongezeka na watu kujenga makazi na kufungua vijiji katika mapito ya wanyama ya Kwakuchinja na maeneo ya mtawanyiko jambo ambalo ni tishio kubwa kwa ustawi wa wanyama.

Inapotokea simba wakati anapita kutoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda jingine wakala wa mifugo basi jamii huweka sumu na wanapokula simba wengine na wanyama wengine kama fisi, bweha na ndege mbalimabli hufa kwa wingi.

Mwaka 2009 katika Kijiji cha Kimotorok waliuawa simba watano ikiwa ni mama, baba na watoto yaani familia nzima na 2015 waliuawa simba watano kwa kula mzoga uliowekewa sumu ikiwa ni mama na watoto wake.

Matukio haya yamekuwa yakijirudia kiasi cha simba waliovalisha kifaa maalum cha utambuzi wa mienendo yao kuuawa, na chanzo kikuu ni wanyama hao kula mifugo wakiwa katika njia kutoka eneo moja kwenda kwingine.

Mtaalamu huyo anaeleza kuwa shoroba ya Kwakuchinja inaendelea kupungua upana wake na sasa wanyama wanapita kwa tabu kwa kuwa kuna makazi na mashamba, huku kukiwa na kikazo kingine cha barabara ya Arusha Babati ambayo kila siku mnyama mmoja huuawa.

Kwa ufuatiliaji wa mwaka jana ulibaini wanyama 380 waliuawa kwa kugongwa na magari, ikiwa ni namba nyingine ya kuendelea kuwapunguza.

Utafiti mbalimbali duniani umeonyesha kuna zaidi ya simba 30,000 kati yake 15,000 wako Tanzania hasa katika ikolojia ya Serengeti, na yapo maeneo duniani simba walishapotea na imebaki historia.

Kazi ya watafiti ni kufanya uchunguzi na kuleta matokeo ya walichokibaini hadharani, tayari wameweka hadharani kile walichokiona na ameshauri hatua za kuchukua kama kujenga njia za chini au juu kwa wanyama kupita, jambo ambalo linahitaji ushiriki wa wadau wote.

Tayari Shirika la Misaada la Watu wa Marekani kupitia mradi wa USAID Protect wamesaidia kuonyesha hali halisi katika eneo hilo, ikiwamo maeneo ambayo wanyama wanapita kwa wingi, ikiwa kutoa takwimu za ajali za barabarani.

Kutokana na umuhimu wa wanyamapori katika uchumi wa Tanzania, ni lazima hatua madhubuti zichukuliwe, vinginevyo wanyama watabaki kwenye visiwa yaani hataweza kuhama kutoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda jingine na madhara ni kuwa na kizazi dhaifu na hata kupotea kabisa.

Katika ikolojia hiyo yapo maeneo yanayohifadhiwa na jamii yaani Wildlife Management Area (WMA), kama ya Burunge iliyoundwa kutokana na vijiji 10 vilivyotoa eneo na sasa vinanufaika na uhifadhi kwa kupata mapato ya Sh. milioni 103 wanazozipangia shughuli za maendeleo na kuachana na uchangishanaji.

Faida za moja kwa moja za wanyama hawa zipo kwa kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Halmashauri ya Babati wanapata fedha zinazotokana na jamii kutunza eneo hilo.

Simba na wanyama wengine ni muhimu sana kwa utalii kwa kuwa wapo watalii wanatoka nchi za mbali kuja kumuona tembo, kufanya utalii wa picha na uwindaji ambao kisheria mtalii anapewa siku 21 na malipo yake ni Dola za Marekani 12,0000 (sawa na zaidi ya Sh. milioni 28), inapotokea mnyama huyu anauawa basi ni harasa kwa taifa, lazima hatua zichukuliwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Utoro unapeperusha azima lengo namba 4



Na Sabato Kasika

**LENGO** namba nne la Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ni kuwapo elimu bora yenye usawa na kutoa fursa kwa wote kujiendeleza ili kumwezesha kila raia kusoma na kujifunza ili wote wafikie vipawa vyao kikamilifu.

Kutokana na hilo, serikali za mitaa zina nafasi ya kuhamasisha elimu ya ufundi stadi katika mikakati ya maendeleo ya kiuchumi na kuhakikisha kuwa mafunzo yanaleta tija katika soko la ajira.

Vilevile serikali za mitaa zinatakiwa kufanye utambuzi ili kuyafikia makundi yalio pembezoni na katika mazingira hatarishi ili yapewe nafasi na kupata elimu na mafunzo yanayokidhi mahitaji yao.

Hata hivyo, kumekuwapo na changamoto kama vile upungufu wa walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambazo zinatakiwa kupatiwa ufumbuzi ili kuondokana na hali hiyo.

Katika harakati za kufikia lengo hilo, serikali za mitaa zimepewa jukumu la kuhakikisha wasichana na wavulana wote wanahitimu elimu ya msingi na sekondari yenye ubora na usawa unaoleta tija ifikapo mwaka 2030.

Madhumuni mengine ni kuongeza mahudhurio ya wanafunzi shuleni, pia kuona kuwa wasichana na wavulana wote wana fursa sawa ya kupata elimu bora ya awali ili iwaandae kwa elimu ya msingi.

Yapo mengi ambayo yanaelezwa kwenye lengo hilo namba nne, lakini suala la utoro ndilo linaloweza kuhatarisha mafanikio kama halitapigwa vita na jamii nzima kwa vile litakwamisha malengo hayo kutimia.

Utoro shuleni ni moja ya tishio la kutimiza mpango huo wa malengo endelevu kama hautadhibitiwa kwa kudhani kwamba wanaohusika ni watu fulani na kumbe ni tatizo la wote.

Serikali ilishaamua kulivalia njuga suala la utoro na imekuwa ikiifanya kampeni za kuihamasisha jamii kuelewa umuhimu wa elimu, kuwafikisha mahakamani wazazi wasiohimiza watoto kwenda shule.

Hata wanaowafanyisha kazi watoto badala ya kuwapeleka shule, na wakati mwingine kuwapo kwa maandamano ya amani yenye lengo la kuhamasisha viongozi wa serikali, walimu, wazazi kuhimiza umuhimu wa elimu.

Kwa hali kama hiyo ni wazi kwamba kila mmoja kuanzia kwa wazazi na walezi wanahusika kukemea vitendo hivyo, ili watoto wahudhurie masomo kwa muda wote bila utoro usio wa lazima.

Wakati akizundua mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka juzi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa anaitaja mikoa inayoongoza kwa utoro ukiwamo Tabora, Geita, Mtwara na Shinyanga.

Mikoa hiyo inatajwa kuongoza kwa utoro wa wanafunzi wa sekondari na kuwataka wakazi wake wakiwamo wazazi na walezi kuhamasisha watoto wao kuhusu umuhimu wa elimu na mahudhurio.

Kutokana na utoro huo, Desemba mwaka jana, Mkurugenzi Msaidizi Msingi na Uendelezaji wa Sera, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Yesse Kanyuma, anasema serikali ipo kwenye utaratibu wa kurekebisha waraka wa kudhibiti utoro.

Waraka huo utabainisha wajibu wa kila mdau, na kwamba ili kudhibiti utoro shuleni, serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha andiko hilo.

Lengo ni kuja na mkakati wa kuhakikisha utoro unadhibitiwa, hivyo waraka utabainisha wajibu wa kila mdau, ukielezea ni namna gani walimu wa madarasa, nidhamu, wakuu wa shule, wanaweza kutimiza wajibu wao katika kukabiliana na utoro shuleni.

Kutokana na mikakati hiyo, ni wazi kwamba kila mmoja anahusika katika kudhibiti utoro kuanzia nyumbani, ndani ya jamii hadi shuleni.

Ikumbukwe kuwa wapo wanafunzi, ambao wanaweza kusingizia kuwa wanaumwa na kutohudhuria masomo na wakati mwingine ni ujanja, pia kuna wanaoaga kwenda shuleni lakini huishia njiani.

Katika mazingira hayo, kuna haja ya kuwapo ushirikiano mkubwa kati ya wazazi, walezi, jamii na walimu, ili kupeana taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kama njia mojawapo ya kudhibiti utoro.

# HEKA HEKA ZA KAMPENI UCHAGUZI MKUU



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, akikabidhi nakala ya ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 kwa mgombea ubunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Sospeter Muhongo, kwenye mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika viwanja vya Bukima, wilayani Musoma Vijijini jana. **PICHA: OWM**



Mbunge mteule wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Fatuma Tofiq, akimwombea kura Diwani wa Kata ya Nzuguni, Aloiyce Luhenga (wa pili kulia waliokaa mbele), kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika uwanja wa Shule ya Msingi Nzunguni B, Dodoma mjini jana. **PICHA PETER MKWAVILA**




Mwenyekiti wa Chama cha United Democratic Party (UDP), John Cheyo akimnadi mgombea ubunge Jimbo la Itilima, mkoani Simiyu kupitia chama hicho, Ngangani Charles, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Kata ya Ruguru juzi. **PICHA: HAPPY SEVERINE**



Mgombea udiwani Kata ya Ngamiani Kaskazini jijini Tanga kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Fahad Abdalah, akinadi sera zake wakati wa ufunguzi wa kampeni za uchaguzi mkuu katika viwanja vya Mwafrika, Barabara ya Nne, jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**



Mgombea ubunge Jimbo la Kibamba, kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Kunje Ngombale Mwiru (kushoto), akiomba kura kwa wauza mboga eneo la Kibamba Hospitali, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mgombea udiwani wa Kata ya Elerai Mkoa wa Arusha kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Yasin Ally, akinadi sera zake wakati wa ufunguzi wa kampeni za uchaguzi mkuu katika kata hiyo, juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Norway yaifagilia Tanzania kielelezo cha amani Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imetajwa kama nchi ya kielelezo cha amani na demokrasia katika Bara la Afrika kutokana na mchakato wa kampeni za uchaguzi mkuu unavyofanyika kwa amani, utulivu na usawa kwa wagombea wa vyama vyote, huku wananchi wakijitokeza kwa wingi kusikiliza sera za wagombea.

Balozi wa Norway nchini, Balozi Elisabeth Jacobsen, aliyasema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, na kuongeza kuwa maandalizi ya uchaguzi mkuu yamefanyika kwa kufuata taratibu za kisheria, huku Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ikishughulikia baadhi ya malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na baadhi ya vyama vya siasa na wadau mbalimbali, jambo ambalo linaifanya Tanzania kuwa kinara wa demokrasia katika mchakato mzima wa uchaguzi," alisema.

Pamoja na masuala ya kisiasa balozi huyo alisema katika mazungumzo yao wamegusia pia masuala ya ushirikiano wa kidiplomasia na kiuchumi hususani katika suala la elimu, afya, nishati na uwekezaji pamoja na biashara baina ya nchi hizo mbili.

Prof. Palamagamba Kabudi alimwomba Balozi huyo wa Norway kuendelea kushirikiana na Tanzania na kumshukuru kwa nchi hiyo kukubali kutoa kiasi cha dola za Marekani milioni 7 kwa ajili ya mradi wa TASAF, jambo litakalosaidia kupunguza umaskini kwa Watanzania hususani katika kipindi hiki ambapo nchi nyingi zimeathiriwa na janga la corona.

Mbali na Balozi huyo wa Norway pia Prof. Kabudi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Sweden nchini, Balozi Anders Sjöberg, ambapo amezungumzia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, haki za binadamu na uhuru wa vyombo vya habari, na kuvipongeza vyombo vya habari nchini kwa kuandika habari za wagombea wa vyama vyote bila ya ubaguzi na ameonyesha kufurahishwa kwake na mwitikio wa wananchi katika mikutano ya kampeni na kuomba maamuzi ya wananchi katika sanduku la kura yaheshimiwe.

Kuhusu suala la haki za binadamu, Prof. Kabudi alisema taswira inayotolewa kuhusu suala hilo haiakisi hali halisi iliyopo nchini, na kwamba Tanzania inaheshimu na kulinda misingi ya haki za binadamu kiasi cha suala hilo kuingizwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ili kikiingia madarakani kitekeleze na kulinda misingi ya haki hiyo.

Katika tukio jingine Waziri Kabudi alipokea nakala za hati za utambulisho za Balozi Mteule wa Uswis hapa nchini, Didier Chassot.

# Ndikilo aridhishwa kiwanda kudhibiti uharibifu mazingira

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema uwekezaji wa kiwanda cha kutengeneza mitungi ya gesi unaofanywa na kampuni ya Lake Group, utaondoa changamoto ya uharibifu wa mazingira ndani na nje ya mkoa wa Pwani.

Ndikilo aliyaeleza hayo mwishoni mwa wiki baada ya ziara ya siku moja ya kutembelea baadhi ya viwanda katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Alisema, kiwanda hicho ambacho ni cha kwanza nchini mitungi itakayokuwa inatengenezwa itawafikia wananchi kwa urahisi na kwa bei nafuu ukilinganisha na inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

"Ukataji miti uliokithiri unakwenda kumalizika uharibifu wa mazingira kutokana na matumizi ya kuni na mkaa, sasa unaisha baada ya Lake Group kuanzisha kiwanda hiki ambacho kwa nchini ni cha kwanza," alisema Ndikilo.

Mkurugenzi wa Lake Oil, Frank Nyabundege, alisema, kiwanda hicho ni kati ya viwanda vinavyomilikiwa na kampuni ya Lake Group kikiwamo cha nondo, mabomba ya maji na cha mitungi ya gesi.

Nyabundege alisema kiwanda cha Lake cylinder (kinachotengeneza mitungi) ni kiwanda pekee Afrika Mashariki kuzalisha mitungi ya gesi, na kwamba kitakapokamilika katika awamu zote kitakuwa na uwezo wa kuajiri wafanyakazi 250 na katika awamu ya kwanza wafanyakazi 25 wamepata ajira rasmi na 90 ni ajira zisizo rasmi.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kutengeneza mitungi 50,000 kwa mwezi na 600,000 kwa mwaka, na kwamba mitungi hiyo ni asilimia 30 ya mitungi inayoagizwa nchini.

Alibainisha kuwa Lake Group kupitia viwanda vyake vitatu vyote vikianza kufanya kazi, vitakuwa na uwezo wa kulipa kodi zaidi ya Sh. bilioni 2.8.

Ndikilo alitembelea pia kiwanda cha kutengeneza dawa za binadamu cha Kairuki, ambacho kikikamilika kitapunguza gharama za kuagiza dawa nje ya nchi.

# Wachimbaji wadogo wapata fursa ya kupata uzoefu nje

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kushoto), akikaribishwa katika maonyesho ya dhahabu na teknolojia yanayoendelea mkoani Geita, alipotembelea banda la Benki ya NBC jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Binafsi wa benki hiyo, Elibariki Masuke. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

SERIKALI imeunga mkono mpango wa kuwasafirisha wachimbaji wadogo na wajasiriamali wa sekta ya madini nchini katika mataifa yanayofanya vizuri kwenye sekta ya madini ikiwamo Zimbabwe, Ghana na Msumbiji ili wakajifunze na kutafuta namna bora zaidi ya kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kiwango cha kimataifa.

Fursa hiyo imetolewa na Benki ya NBC, huku serikali ikisema iko tayari kushirikiana na benki hiyo katika kufanikisha ziara hizo.

Akizungumza alipotembelea banda ya benki hiyo, lililopo kwenye viwanja vya maonyesho ya dhahabu na teknolojia yanayoendelea mkoani Geita, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema pamoja na kushirikiana kufanikisha ziara hizo, serikali itashauriana na wadau wote wakiwamo wachimbaji hao ili kuongeza tija katika safari hizo.

"Ili safari hizi ziwe na tija zaidi kwa walengwa, serikali ipo tayari kushirikiana na pande zote wakiwamo wachimbaji ili kufahamu nchi sahihi ambazo zimefanya vizuri kwenye sekta hii ili walengwa wapate wasaa wa kujifunza mambo ambayo yatawasaidia zaidi...hivyo nawapongeza sana benki ya NBC kwa mpango huu," alisema Biteko.

Mkurugenzi wa Idara ya wateja binafsi wa benki ya NBC, Elibariki Masuke, alisema mpango huo umekuja kufuatia mafunzo maalum ya siku tatu yaliyotolewa na benki hiyo kwa wachimbaji wadogo na wajasiriamali katika sekta ya madini yaliyofanyika kwenye maonyesho hayo.

"Malengo ya safari hizo haswa ni kutusaidia sisi sote yaani benki ya NBC na wateja wetu kwenye sekta ya madini ili kwa pamoja tukabadilishane uzoefu na wenzetu ambao pia wanafanya vizuri kwenye sekta hii. Kupita safari hizo tunatarajia makundi haya mawili wachimbaji watajifunza namna mpya na bora zaidi ya kuendesha biashara zao ikiwamo namna ya kulifikia soko," alibainisha.

Alisema kupitia mafunzo hayo, benki hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine wamebaini baadhi ya changamoto zinazowakabili wadau hao, hivyo kuwajengea uelewa wa namna ya kukabiliana na changamoto hizo wao wenyewe huku pia benki hiyo ikiahidi kutumia changamoto hizo katika kubuni huduma mahusus zinazolenga kuziondoa kabisa.

"Aidha kwa sasa benki ya NBC ipo kwenye hatua za mwisho kuzindua huduma maalum kwa ajili ya wadau wa sekta ya madini nchini ambayo kwa kiasi kikubwa inalenga kujibu changamoto zilitojwa na wachimbaji wadogo pamoja na wajasiriamali wakati wa mafunzo yetu," alisema.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo pamoja na kuishukuru benki hiyo walisema kupitia mafunzo hayo wameweza kufahamu namna bora ya kuweka mipango na mikakati ya kukuza biashara zao, namna ya kutafuta masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi, mambo yanayoangaliwa na benki kabla ya kupatiwa mkopo pamoja na kufahamu sababu zinazosababisha biashara zao zife.

HABARI KITAIFA

# Lugha chafu zawakera wanawake sokoni

Na Christina Mwakangale

LUGHA zisizo na staha, elimu duni ya utunzaji fedha na kupanga bajeti ni kati ya changamoto zinazowakumba kinamama wafanyabiashara kwenye masoko.

Ofisa Utawala wa Asasi ya Equality for Growth (EfG), Evah Busembo, aliyasema hayo hivi karibuni jijini Dar es Salaam wakati akielezea mafanikio na changamoto katika mkutano uliokutanisha asasi za kiraia zilizoshiriki mradi wa changamoto za kueleza habari 'Story Telling Challenge'.

**Mrejesho uliotolewa na washiriki wa mradi huo, umebainisha umuhimu wa shughuli za asasi hizo kusikia kwenye vyombo vya habari, ili kufikisha ujumbe.**

Alisema walibaini hayo katika masoko 18 yaliyopo Wilaya ya Ilala na Temeke, jijini Dar es Salaam, lengo likiwa ni kuwapa elimu kinamama wanaofanya shughuli za kujipatia kipato sokoni na kutunza fedha.

"Kinamama wanaofanya shughuli zao sokoni wanapata kipato kizuri kwa siku, ila namna ya kutunza hizo fedha na kutambua kuwa wanapata faida ndio changamoto, wanakuwa na matumizi ambayo ni mengi na hawajayapanga," alisema Buhembo na kuongeza.

"Tulikutana na lugha wanazopewa zisizo na staha wanaitwa majina yasiyo na heshima kinamama hawa, tunaendelea kutoa elimu kwa jamii itambue kuwa kazi hii ni kama shughuli nyingine, tuwape heshima kinamama."

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa MediaSpace, Vicensia Fuko, akifungua mkutano huo ulioshirikisha asasi hizo, waandishi wa habari na wataalamu wa takwimu mtandaoni, alisema kuwa mradi huo ulilenga kuinua sauti za makundi ya kijamii yanayofanya vizuri shughuli za kuwakwamua Watanzania kiuchumi.

"Ulikuwa mchakato mrefu wa kuzipata asasi hizi ambazo zina ujumbe mzuri kwa jamii na kuelimisha, lakini wanakosa jukwaa la kusikika au kuwasogeza mbele, wapige hatua zaidi," alisema Fuko.

Alisema mrejesho uliotolewa na washiriki wa mradi huo, umebainisha umuhimu wa shughuli za asasi hizo kusikia kwenye vyombo vya habari, ili kufikisha ujumbe.

Pia alisema kuwa mradi huo ulijikita kufanya kazi na waandishi wa habari ili kukuza uhuru wa habari na uelewa.

"Kuna vijana wadogo ambao wepesi wa kutuma taarifa mtandaoni, ziwe za kweli au uongo, lakini jamii utakuta hata kama ni uongo wanazishabikia, tukaona tunawapaje elimu kundi hili ambao ni waandishi jamii," alisema Fuko.

Alisema ukuaji wa teknolojia umeongeza fursa ya jamii kuhabarisha, ingawa kunahitajika usahihi na mafunzo kwa wanaotoa taarifa hizo.



Mzalishaji Mkuu wa Kiwanda cha Said Salim Bakhresa Ltd, George Otieno (aliyeinama chini), akiwaelekeza jambo baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa zinazotengenezwa kwa unga wa ngano wa kampuni hiyo, walipotembelea kiwanda cha Buguruni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ataka watoto kusikiliza redio za dini

Na Christina Haule, MOROGORO

MHASHAMU Askofu wa Jimbo la Katoliki Morogoro, Telesphory Mkude, amewataka wazazi hasa wa kike kuendelea kuwalea watoto kimaadili, ili wamjue Mungu na kujiepusha na mambo yasiyofaa.

Askofu Mkude alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Ofisi ya Redio Maria, Kanda ya Morogoro zilizopo kwenye Kanisa Katoliki la Mtakatifu Maria Modeko, mkoani hapo. Alisema siku zote mama anapaswa kutambua kuwa ndiye katekista wa kwanza wa mafundisho ya mambo ya Mungu kwa mtoto kabla wa kanisani.

Kadhalika, alisema wazazi wananafasi kubwa ya kuwalea watoto katika maadili mema ya njia za kumpendeza Mungu.

"Sisi sote ni watoto wa Mungu na kwa sababu Yesu ni mwana wa Mungu, sisi sote ni wana wa Mungu na hivyo ni wana wa Mama Bikira Maria...hivyo wazazi hawana budi kuwalea watoto kama Mama Maria alivyomlea vyema mtoto Yesu," alisema.

Aliwataka wazazi wawazoeshe watoto wao kusikiliza redio za dini ili wajifunze mambo muhimu ya kumjua Mungu na kuyaishi.

Alisema redio za kanisa zina nafasi kubwa ya kuielimisha jamii ikiwamo watoto hata wawapo nyumbani mambo ya kumpendeza Mungu.

Naye Katibu wa Halmashauri Walei Parokia ya Modeko, Martha Mkoma, alipongeza uongozi wa Redio Maria makao makuu kwa kufungua ofisi katika Parokia ya Mtakatifu Maria - Modeko na kuwa heshima kubwa kwao wanaparokia ya Modeko kwa kuukaribisha utume wa Redio Maria.

## Waomba mafunzo nishati mbadala

Na Yasmine Protace

KIKUNDI cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam, kimeomba wabunge watakaofanikiwa kuchaguliwa na wananchi, mwaka huu, wawaandaliе wananchi mafunzo ya kutengeneza taka kuwa mkaa na waache kukata miti ovyo.

Pia wameomba halmashauri nazo zianzishe mafunzo ili taka zitumike kwa ajili ya kuokoa ukataji wa mkaa.

Hayo yalisemwa na Bishagazi Selemani, Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam katika mafunzo yaliyotolewa kwa wanakikundi jinsi ya kutengeneza mkaa kwa kutumia taka za majumbani na chenga za mkaa.

"Kukitolewa mafunzo jinsi ya kutumia taka za nyumbani, taka za mitaani na chenga za mkaa kutengeneza mkaa, tatizo la ukataji miti litapungua," alisema.

Aliongeza kuwa kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, kimetoa mafunzo ya kutengeneza mkaa kwa kutumia taka na chenga za mkaa.

Alisema mafunzo hayo yametolewa katika vikundi 12, ambapo lengo ni kuzibadilisha taka kuwa fursa.

Alisema mafunzo ya kutengeneza nishati mbadala waliyapata kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), na wao wameyatoa kwa washiriki 65 kutoka vikundi 12 vilivyopo katika Gongo la Mboto Manispaa ya Ilala.

Alisema ukataji miti imekuwa ukisababisha hali ya ukame na takwimu zinasema asilimia 60 ya wakazi wa Dar es Salaam wanatumia mkaa ambao unatoka Singida.

## Ukaguzi wa mizani kwa kushtukiza waja

Na Mwandishi Wetu, GEITA

WAKALA wa Vipimo nchini (WMA), umeanza kufanya operesheni za kushtukiza kukagua mizani inayotumika kupima dhahabu, ili kuhakikisha serikali inapata kodi yake stahiki na kuwachukulia hatua za kisheria wale wanaojaribu kuchezea mizani.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Vipimo wa WMA Geita, Chrispinus Aloyce, wakati akizungumzia ushiriki wa taasisi yake kwenye maonyesho ya tatu ya madini ambayo yanafanyika katika viwanja vya Bomba Mbili Mwatulole, mkoani Geita.

Alisema WMA inamchango mkubwa katika sekta ya madini, ambapo biashara hiyo haiwezi kufanyika bila kuwa na mizani sahihi na iliyohakikiwa na wakala ili kuweza kutambua uzito halisi wa dhahabu inayonunuliwa au kuuzwa.

Alisema jukumu kuu la WMA katika sekta hiyo ni kuhakikisha mizani yote inayotumika kuuzia na kununulia vito na madini inahakikiwa na inapima madini kwa usahihi na pia taasisi hiyo inatoa ushauri wa kitaalamu juu ya mizani zinazopaswa kutumika kuuzia madini.

Alisema baada ya uhakiki wa mizani hiyo kukamilika huwekewa alama maalumu ambayo inaonyesha utambuzi kuwa mizani imehakikiwa na inafaa kutumika kununulia madini.

# Kunje kuwafuta machozi waliobomolewa Kibamba

**Na Sabato Kasika**

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Kibamba, jijini Dar es Salaam kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Kunje Ngombale Mwiru, ameahidi kifuta machozi kwa wakazi wa jimbo hilo, waliomolewa nyumba katika upanuzi wa barabara ya Morogoro.

Kunje alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki walipotembelea maeneo mbalimbali ya jimbo hilo, kusalimiana na wananchi ikiwa ni sehemu ya maandalizi yake ya kujiandaa kufanya kampeni.

Alisema, akichaguliwa atapeleka bungeni hoja ya kutaka watu wote waliovunjiwa nyumba wapewe kifuta machozi kwa vile wanahitaji kusaidiwa badala ya kuachwa walivyo wakiendelea kusononeka.

**Yapo mengi ambayo chama kimeahidi kupitia katika ilani, miongoni mwake ikiwa ni kuboresha maisha ya Watanzania, hasa wanyonge kwa kuwapa mikopo bila riba wala dhamana.**

"Mkinichagua nitafanya mengi kwa ajili ya maendeleo ya jimbo hilo, ikiwamo kupeleka hoja bungeni ya kutaka wale wote waliovunjiwa nyumba wapewe kifuta machozi, kwani wameumia," alisema Kunje.

Mgombea ubunge huyo alifafanua kuwa siyo rahisi kufanya tathmini, kwa madai kwamba nyumba zilishavunjwa, hivyo kinachotakiwa ni kila mhusika kipewa kifuta machozi kutokana na adha aliyopata.

Alisema, yapo mengi ambayo chama kimeahidi kupitia katika ilani, miongoni mwake ikiwa ni kuboresha maisha ya Watanzania, hasa wanyonge kwa kuwapa mikopo bila riba wala dhamana.

Aidha, alisema, akichaguliwa ataweka mikakati ya kuhakikisha wajasiriamali wanapata shilingi milioni moja za mkopo bila riba wala dhamana ili waweze kufaidi matunda ya nchi yao.

"Watu wa hali ya chini wanahangaika sana kupata mikopo kutokana na masharti ya riba na dhamana...wanajikuta wanakwama na kuendelea kubaki maskini, lakini sisi SAU hilo halitakuwapo tena," alisema.

Alisema, kutakuwa na utaratibu maalum wa kumtambua kila mmoja atakayekopeshwa ili usiwepo udanganyifu wa aina yoyote, kwamba, mkopaji akipewa shilingi milioni moja, atarejesha kiasi hicho baada ya mwaka mmoja.

"Hayo yamo katika ilani ya chama chetu, lengo ni kuwainua wanyonge wote, hivyo hatuwezi kuwapa mzigo wa riba au kikwazo cha kuweka dhamana ya nyumba ama kitu kingine, bali tutaweka mfumo ambao ni rahisi kwa kila mmoja kukopa," alisema.



Mamalishe Fasia Bakari akisonga ugali kwa ajili ya mlo wa mchana kwa wateja wake, kwenye eneo la wazi la Kiluvya, jijini Dar es Salaam juzi, bila ya kuchukua tahadhari ya vumbi, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za walaji. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wananchi watakiwa kushiriki kwenye kampeni kusikiliza sera

**Na Christina Mwakangale**

JAMII imetakiwa kuhudhuria kampeni za uchaguzi zinazoendeshwa na wagombea kupitia vyama mbalimbali vya kisiasa, ili kufahamu sera, ilani na vipaumbele vyao kwa ajili ya kufanya uamuzi sahihi ndani ya sanduku la kura, Oktoba 28, mwaka huu.

Pia, wameshauriwa kuuliza maswali kwa wagombea hao, kila wanapopata fursa hiyo kwa kuwa ni haki yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Sauti ya Mama Africa Foundation (SAMAFO), Tabitha Bugali, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki akielezea fursa ya wananchi na ushiriki wao katika uchaguzi mkuu.

Alisema kupitia mikutano ya hadhara ya kampeni, watatambua wa kumpa kura siku ya kupiga kura na kumchagua kiongozi bora na si bora kiongozi.

"Elimu kwa wapigakura, ambao wananchi wenye sifa za upigaji kura, inasaidia kuwapa mwanga na uhuru wa kuchagua wanachoona kinafaa," alisema Bugali.

Alisema kuwa shirika hilo limeyafikia makundi maalumu katika jamii, yakiwamo ya wanawake, watu wenye ulemavu, vijana na wazee katika maeneo tofauti ya jijini Mbeya.

Bugali alisema maeneo hayo ni katika Kata ya Forest, Mbalizi Road, Mabatini, Mbeya Vijijini, Utengule-Usongwe na Nsalala.

"Tumeelimisha Kata ya Forest kwenye mitaa saba, mitaa sita Mabatini na wiki ijayo tutakuwa Kata ya Mbalizi Road yenye mitaa minne," alisema Bugali.

Kadhalika, Bugali alisema elimu wanayowapa wapigakura ni kufahamu sifa za mpigakura, umuhimu wa kitambulisho cha mpigakura, kituo cha kupigia kura na kuzingatiwa muda wa kuanza na kumaliza upigaji kura.

"Tunasisitiza jamii kuheshimu makundi maalumu wapewe kipaumbele wasikae foleni ndefu, hasa wenye ulemavu, wajawazito, wenye watoto na wazee," alisema Bugali.

## Devota Minja kufungua duka la dawa hospitali

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa tiketi ya CHADEMA, Devotha Minja, amesema akipata ridhaa ya kuliongoza jimbo hilo, atatumia fedha za miaka miwili za mfuko wa jimbo Sh. milioni 57 kwa mwaka kufungua duka la dawa kwenye geti la Hospitali ya Rufani Mkoani hapa ili wananchi wapate dawa kwa wepesi na kwa bei rahisi.

Minja alisema hayo wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho zilizofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege Manispaa ya Morogoro.

Alisema licha ya kuwa na hospitali, lakini upatikanaji wa dawa umekuwa mgumu na kwamba kwa kuweka duka la dawa la serikali kutasaidia wananchi kupata dawa zote wanazoandikiwa hospitali.

Alisema atahakikisha anajenga hospitali ya wilaya kwani haipo na kama ipo haina uwezo wa kutoa huduma ukiwamo upasuaji licha ya eneo kuwa mbali na makazi ya watu.

Naye mgombea ubunge wa Jimbo la Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, aliwataka wakazi wa Morogoro kumchagua Devotha Minja kuwa mbunge wao ili waone mabadiliko.

## Mkakati kuongeza uzalishaji korosho

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeanza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao la korosho nchini kutoka tani 315,000, ili kufikia tani milioni moja ifikapo mwaka 2023 lengo ikiwa kukuza uchumi wa wakulima.

Kupitia mkakati huo Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania pamoja na halmashauri imeamua kuendesha mafunzo na kutoa mbinu za kilimo bora cha zao la korosho hapa nchini.

Akizungumza katika mafunzo ya kilimo bora cha korosho yaliyohusisha maofisa ugani na wakulima katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, Ifakara, Malinyi na Ulanga, mratibu wa zao la korosho kutoka TARI Naliendele, Dk. Geradina Mzena, alisema lengo la uzalishaji uongezeke kutoka mikoa mitano inayolima korosho hivi sasa na kufikia mikoa 17.

Alihitaja mikoa iliyowekewa mikakati ya kuongeza uzalishaji wa zao la korosho ni Morogoro, Iringa, Dodoma, Singida, Tabora, Katavi, Kigoma, Songwe, Ruvuma Mbeya, Kilimanjaro na Njombe.

Naye Mkuu wa Kituo cha Morogoro kutoka Bodi ya Korosho Tanzania, Luseshelo Silomba, alisema ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa wakulima wa korosho ni lazima kuunganisha nguvu za pamoja kwa kuanzisha vyama vya msingi ili kuwa na umoja wenye nguvu na kupata mikopo katika taasisi za fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo hicho cha korosho.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 22, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12



CWT jiongezeni, wanachama wanahitaji kujua ujasiriamali

# MZAZI INAKUHUSU

- Mama ukijifungua ndani ya saa moja uwe umenyonyesha
- Mgusishe mtoto chuchu hata kama hazitoi maziwa

NA CHRISTINA MWAKANGALE

MARA nyingi kinamama wakijifungua familia au jamii huamini kuwa ili maziwa yatoke ni lazima kula vyakula vya aina fulani, akiwa ni pamoja na uji wenye pilipili mtama na mbegu za mafuta kama alizeti.

Yote hayo, wataalamu wanasema hayasababishi mama aliyejifungua kuanza kutoa maziwa kwa vile uzalishaji na utoaji maziwa ni kazi inayofanywa na ubongo na hisia hivyo si lazima kula pilipili manga.

Dk. Sifa Eli, kutoka Hospitali ya Magomeni jijini Dar es Salaam, akizungumza na Nipashe kuhusu maziwa na unyonyeshaji watoto wachanga anasema ni lazima ufanyike ndani ya saa moja baada ya kujifungua na mama ahakikishe kuwa amemnyonyesha mtoto.

"Mtoto anapozaliwa baada ya saa moja anyonyeshwe hata kama maziwa ya mama hayatoki."

Anaonya kuhusu dhana au fikra potofu kwa baadhi ya kinamama kwamba, anapotoka kujifungua maziwa yanakuwa hayajaanza kujitengeneza na kutoka.

Anasema, msongo, furaha kupitiliza hupoteza maziwa na iwapo mama aliyejifungua akipata msongo wa mawazo au furaha iliyopitiliza anaweza kusababisha uzalishaji wa maziwa kutofanyika ipasavyo na kwa wakati.

"Kinachofanya maziwa yaanze kutoka ni ubongo, hisia, baadhi wanadhani hadi mama ale vyakula vya aina fulani, au uji wa pilipili manga si lazima. Cha msingi, awe huru kifikra bila msongo," anasema Dk. Sifa.

Anataja baadhi ya mambo yanayoweza kusababisha maziwa yasitoke kuwa ni pamoja na mama kuwaza kupindukia mathalani, wapi atapata pesa ya kula, matunzo ya mwanawe na matokeo yake ni kuzuia maziwa kujitengeneza.

Anasema pia maziwa ya mama yanaweza yasitoke kutokana na baadhi ya kinamama kutumia dawa za tiba mbalimbali, bila kufuata ushauri wa kitabibu na kuwakumbusha kuwa kama unayenyonyesha usinunue dawa na kumeza ila cha muhimu ni kufika hospitalini au kituo cha afya na daktari atafahamu dawa gani atampatia kwa kuwa ananyonyesha.

"Mtoto agusishwe chuchu saa moja ya kwanza," Dk. Sifa anafafanua na kuongeza kwamba zipo sababu ambazo zinaweza kusababisha maziwa ya mama aliyetoka kujifungua yasitoke, akitaja msongo wa mawazo au kuwa na furaha kupindukia baada ya kumuona mwanawe kuchangia.

Anaainisha kwamba, mama ambaye hajajiandaa kunyonyesha, anaweza kusababisha maziwa yasitoke sababu yanaanza kutokana na hisia baada ya taarifa kupelekwa ubongoni, kuwa mtoto amezaliwa.

Kadhalika anasema saa ya kwanza ya mwanzo mtoto atakapozaliwa apelekwe kwenye ziwa chuchu ili aanze kunyonya, aiguse hata kama hayajaanza kutoka. Hatua hii itapeleka ujumbe moja kwa moja kwenye ubongo kwamba mtoto amezaliwa hivyo maziwa yatengenezwe.

Sifa anaongeza kuwa, mama akichelewa kunyonyesha maziwa yatachelewa pia kuanza kutoka na kuwataka kinamama waliotoka kujifungua kuwaweke watoto wao kwenye chuchu mara kwa mara ili ujumbe uende mara nyingi ubongoni maziwa yatengenezwe, ndani ya nusu saa yanategemewa kuwa yanatengenezwa.



Kunyonyesha baada ya kujifungua kunasisimua maziwa kutoka, pia mama kuwa na amani na utulivu wa akili ya mwili. **PICHA: MTANDAO**

> Kinachofanya maziwa yaanze kutoka ni ubongo, hisia, baadhi wanadhani hadi mama ale vyakula vya aina fulani, au uji wa pilipili manga si lazima. Cha msingi, awe huru kifikra bila msongo

### MZAZI USILALE FOFOFO

Aidha, Sifa anasema wakati wa usiku mama anayenyonyesha hatakiwi kulala usingizi muda mrefu au kwa saa nyingi, kwa kuwa itasababisha uzalishaji wa maziwa kupungua.

"Kulala fofofo, yaani mama anasema usiku na mwanangu tumelala usingizi mzito hadi asubuhi hii sawa. Mama unayenyonyesha asilale usiku kucha, nyonyesha kila mara, usiku na mchana," anahimiza Dk. Sifa.

Anawataka waliojifungua kwa njia ya upasuaji kunyonyesha watoto wao katika muda wa saa moja.

"Kikubwa ni mama kujiamini hata kama umefanyiwa upasuaji utasaidiwa na wahudumu wa afya ili uendelee kunyonyesha, saa ya kwanza ni muhimu sana kwa maendeleo na mchakato wote wa ukuaji."

### SAA MOJA UKIJIFUNGUA

Dk. Sifa anahimiza kumnyonyesha mtoto saa moja baada ya kuzaliwa kuwa ni lazima kwa michakato ya ukuaji na ni hatua muhimu ya mwanzo ya kujenga kinga imara katika mustakabali wa kukua kwa watoto.

Katika ngazi za kimataifa, kutokana na umuhimu wa kunyonyesha Umoja wa Mataifa (UN) uliitangaza wiki maalumu ya unyonyeshaji duniani inayofanyika kuanzia Agosti Mosi kila mwaka, kutoa msisitizo kwa jamii kuunga mkono kuwanyonyesha watoto wachanga kwa afya ya mataifa na dunia kote ili kuwa na watu wenye afya.

Aidha, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO) linatathmini kuwa, ongezeko la kiwango cha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee, linaweza kuokoa maisha ya watoto 820,000 kila mwaka.



### MAZIWA NI LISHE

Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo ya Shirika la Chakula na Lishe (TFNC), Sikitu Kihinga, anasema katika Siku ya Unyonyeshaji Duniani mwaka huu, anakumbusha kuwa miezi sita ya kumlisha mtotto maziwabila kumpa chakula kingine ni kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa na kukuza afya ya akili.

Anaungwa mkono na Ofisa Mtafiti Mwandamizi wa shirika hilo, Gelagister Gwarasa, anayeeleza kuwa madhara ya kumlisha vyakula vingine badala ya maziwa mtoto wa chini ya miezi sita,

ni utapiamlo, mzio au aleji, kuhara na kupunguza uhusiano kati ya mama na mtoto.

Katika hilo, Ofisa Lishe wa UNICEF-Tanzania, Tuzie Edwin, anasema kukosa muda wa kunyonyesha watoto ni changamoto inayowakabili wazazi wanaofanya kazi na kuwataka waajiri kuweka mazingira hata ikibidi kuwajengea eneo kwa ajili ya kinamama kunyonyesha.

"Licha ya jamii kuelewa umuhimu wa mama kumnyonyesha mtoto lakini bado kuna changamoto mbalimbali ambazo mara nyingi zinakwamisha utekelezaji wake," anasema Edwin.

"UNICEF tuna chumba maalum kwa ajili ya kinamama kunyonyesha watoto wao, lakini kukamua maziwa. Tumezingatia mazingira ambayo ni rafiki kwa mama na mtoto pia.Tunaiasa jamii, familia na serikali kuhamasiha mazingira rafiki kwenye sehemu za kazi, ili kufanikisha kumnyonyesha motto miezi sita."

### FAIDA ZA KUNYONYESHA

Umoja wa Mataifa, unazitaja kuwa ni pamoja na kuleta afya, kinga imara, kuimarisha hisia kati ya watoto na kinamama lakini huweka mfumo endelevu wa chakula kwa watoto.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus, katika siku ya unyonyeshaji anasema kinamama wanahitaji msaada ili kuanza na kuendelea kunyonyesha.

"Wakati unyonyeshaji ni mchakato wa asili, lakini sio rahisi wakati wote," anasema Ghebreyesus.

Pia anatoa wito kwa serikali kulinda na kuongeza fursa za kupata ushauri nasaha kuhusu unyonyeshaji.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA

# CWT jiongezeni, wanachama wanahitaji kujua ujasiriamali

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) ni moja ya taasisi za wafanyakazi zenye jukumu la kusimamia wajibu, haki na maslahi ya walimu na kuwajengea mustakabali mwema wanachama wake na taifa pia.

CWT imekuwa kiungo katika jitihada za kuwaunganisha walimu na serikali ili kuhakikisha walimu wanapata haki zao kwa kuzisikiliza na pia kuziwasilisha hoja, kutetea maslahi, kufikisha madai na ushauri unaotolewa na walimu kwa serikali na wadau wengine ili yafanyiwe kazi.

Zipo changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu hapa nchini, mojawapo ni ugumu wa maisha ambao wakati mwingine limekuwa tatizo likiathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao kwenye vituo vya kazi.

Walimu kwa upande wao wanawajibika kuhakikisha wanakabiliana na changamoto hiyo ya kiuchumi, lakini kwa upande mwingine, chama cha walimu kama mdau na mtetezi wao kinapaswa kuchukua hatua za kuwasaidia wanachama katika nyanja ya kiuchumi kwa kuwasaidia walimu kujua na kujikita kwenye ujasiriamali. Hivyo wanahitaji semina za ujasiriamali na mbinu za utafutaji ili kuwaonyesha na wenyewe kuziona zilipo fursa za kiuchumi.




Mwalimu anafundisha darasani, lakini baada ya kazi anahitaji kuwa mjasiriamali. **PICHA: MTANDAO**

> Mwalimu ni kioo cha jamii kutokana na majukumu anayoyatekeleza na manufaa yake kwa jamii na nchi kwa ujumla. Thamani ya mwalimu itaendelea kukua pale anapokuwa na mafanikio ya kiuchumi pia

Mwalimu ambaye ni mwanachama wa CWT anachangia asilimia mbili katika mshahara wake, ili kuendesha shughuli za chama. Ipo haja sasa ya mwanachama anayechangia fedha zake aanze kunufaika kiuchumi kwa kupata mafunzo na semina za ujasiriamali kutoka kwa wataalamu wa uchumi wanaogharamiwa na CWT.

Uongozi wa CWT taifa uamke sasa uweke utaratibu wa kuhakikisha kila mwanachama wao popote alipo anafikiwa na semina za ujasiriamali ili kumsaidia kujikomboa kiuchumi na kumalizana na changamoto za umaskini.

Viongozi wa CWT Taifa watafute wabobezi wa masuala ya ujasiriamali, mbinu za utafutaji, uwekezaji na uchumi kwa ajili ya kuwafundisha na kuwaonyesha walimu fursa mbalimbali wanazoweza kuzitumia katika kukuza uchumi ili kuwapunguzia ugumu wa maisha.

Michango wanayochangia itenge asilimia kadhaa kwa ajili ya kugharamia mafunzo na semina hizo. Wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa wamekuwa na utaratibu wa kujifunza mara kwa mara mbinu za kiuchumi na kibiashara ili waendelee kufanikiwa zaidi kiuchumi kupitia wataalamu wa uchumi na ujasiriamali.

Aidha, njia hiyo inapaswa kutumiwa na viongozi wa CWT ili kuwasaidia walimu kuwa na uelewa wa kutosha wa namna bora wanavyoweza kujikomboa kiuchumi kupitia semina na mafunzo ya ujasiriamali na uchumi.

Mwalimu ni kioo cha jamii kutokana na majukumu anayoyatekeleza na manufaa yake kwa jamii na nchi kwa ujumla. Thamani ya mwalimu itaendelea kukua pale anapokuwa na mafanikio ya kiuchumi pia. Kutokana na ukweli kuwa hakuna mshahara unaotosheleza mahitaji ya binadamu, na pia kuwapo na umuhimu wa kuwa vyanzo vya mapato zaidi ya kimoja, walimu nao hawana budi kuwa na shughuli nyingine za kujiongezea kipato tofauti na mshahara wanaoupata katika taaluma yake.

Vilevile, CWT imeanzisha benki ya walimu ya Mwalimu Commercial Bank (MCB) ambayo ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia walimu kiuchumi. Kwa kutumia wataalamu wa MCB, mafunzo ya ujasirimali yanaweza kutolewa kwa mafanikio makubwa kwani taasisi za fedha zina wajibu wa kuwafundisha wateja wao ili kuwainua kiuchumi. Viongozi wa CWT wawajibike kuhakikisha walimu wananufaika moja kwa moja na benki yao kwa kujengewa uwezo kupitia mafunzo ya ujasiriamali na uchumi.

Katika kujikomboa kiuchumi, walimu wamekuwa wakikopa mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha hasa benki na wanapaswa kuwezesha kiuchumi kwa kukopeshwa mikopo yenye riba nafuu ili kuwekeza mikopo hiyo katika nyanja za kilimo, ufugaji na biashara ili kuinua hali za kiuchumi za walimu.

Benki ya Walimu inapaswa kuwa chachu ya kuwakomboa walimu kwa kuhakikisha inatoa mikopo yenye riba nafuu kwa wanachama wake ili kuwasaidia walimu kuboresha maisha yao.

Endapo walimu watapata mafunzo ya mbinu za utafutaji, ujasiriamali na uchumi, vilevile kukopeshwa mikopo yenye unafuu kutoka benki yao, hali za maisha za walimu zitaimarika na kuwa bora zaidi.

MCB iwe na manufaa kwa walimu kwa kuhakikisha inatoa motisha kwa wanachama kwa kuwakopesha mitaji yenye riba nafuu ili waanzishe, kukuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi.

Aidha, walimu waelimishwe faida za kuwa wanahisa wa MCB kama njia ya kujiimarisha kiuchumi, CWT ikumbuke ina deni la kuwasaidia walimu katika nyanja ya kiuchumi.

Naamini kabisa, kutokana na uongozi Rais wa CWT Mwalimu Leah Ulaya, Katibu Mkuu Mwalimu Deus Seif na viongozi wengine wa kitaifa, uwezeshwaji wa walimu kuiuchumi utapewa msukumo wa kipekee katika kuhakikisha hali za wanachama zinaimarika kupitia uanzishwaji wa shughuli za ujasiriamali na kiuchumi kwa ustawi wa wa taifa.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**

**Maoni: 0765-409249**

TEKNOLOJIA

# Pasipo matumizi sahihi ni hatari kwa watumiaji

NA MWANDISHI WETU

KATIKA kipindi ambacho kulikuwa na matumizi makubwa ya huduma za mitandao zinazopatikana kupitia simu na kompyuta ni wakati wa mlipuko wa COVID-19 ulioripotiwa nchini kuanzia Machi 17, mwaka huu.

Wakati huo matumizi ya simu na kompyuta kwa ajili ya mawasiliano iwe ya kujitafutia habari, ya kikazi ofisini, biashara, huduma za kijamii na mikutano mubashara ya kimataifa na kitaifa yalikuwa hayakwepeki, hivyo iliwalazimu watumiaji hasa wa kawaida kujiunga na vifurushi vyenye gharama tofauti.

Pia mawasiliano ya mitandao yalitegemewa na taasisi za elimu ambazo ziliwafundisha kwa njia ya madarasa mtandao.

Watoto hao wa shule za misingi hadi wanavyuo kwa takribani miezi mitatu walikuwa nyumbani, ili kuepusha kuenea kwa kasi virusi vya corona.

Mfano wa mikutano iliyofanyika kwa njia za mtandao ni pamoja na ya kikanda, kimataifa ukiwamo ile ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na pia Umoja wa Mataifa nao ulikuwa ukifanya mikutano kwa njia ya mtandao huku mamilioni ya wafanyakazi pote duniani na wengine mpaka sasa wakifanyia kazi nyumbani kwao.

Aidha, miamala ya fedha inayofanywa kwa njia za kielektroniki nayo ikipewa nafasi.


Pamoja na athari zilizojitokeza kwa kipindi hicho hasa kwa mtu mmoja mmoja, taasisi, kampuni na mashirika ni wazi kulikuwa na fursa zaidi za kiuchumi kwa kampuni zinazotoa huduma za mitandao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Zaina Foundation, Zaituni Njovu, akizungumza hivi karibuni kwenye mafunzo ya wanahabari wanawake ambayo yalilenga kuwaongezea ujuzi, kulinda vifaa vya kazi pamoja na kuzingatia usahihi wa vyanzo vya habari mitandaoni, anasema kutumia mitandao ni jambo jema lakini usalama kwanza.

Anasema matumizi ya mtandao, ni lazima yahakikishe kuwa yana ulinzi, kuna faragha na kwa kuwa wanawake ni muhimu.

Zaituni anasema lengo la taasisi yao ni kuwawezesha wanawake kwa kuwapa ujuzi wa namna ya kuhakikisha usalama katika matumizi ya mtandao kwenye ulimwengu wa kidigitali, ikizingatiwa kuwa wengi hawajajihusisha kikamilifu na Teknolojia ya Mawasiliano (IT).

"Haki ya kupokea, kutuma, kutoa taarifa ni ya kila mmoja. Lakini tunahitaji kuwapo usalama wa matumizi ya mtandao, kulindwa kwa faragha, kwa kuwa wanawake ni kati ya waathiriwa wakubwa wa picha zisizo na maadili zikisambazwa mitandaoni bila mtu kujua. Usiri wa data zako ni muhimu, ili zisidukuliwe," anasema Zaituni.



Wateja wanahitaji ulinzi wa taarifa za mawasiliano na faragha wanapotumia mitandao. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Anasema mteja anayejiunga na huduma za mtandao ana haki ya kulindwa usalama wake, kupata huduma ya uhakika bila kukatikakatika na iwapo inatokea tatizo la kiufundi, taarifa itolewe kwa mtumiaji ili kufahamu anapitia kipindi gani na namna ya kujiwekea utaratibu.

"Mtumiaji ameamua kujiunga na kifurushi cha siku au hata wiki, lakini baada ya muda unaambiwa mtandao wa kampuni fulani haupatikani bila taarifa yoyote kabla ni haki yake kupata taarifa, wakati wowote siyo kushtukizwa," anasema Zaituni.

Anafafanua kwamba mafunzo hayo ambayo ni ya awali kutolewa kwa wanahabari, yanawaongezea ujuzi ili kukabiliana na changamoto zilizopo mtandaoni pamoja na kujiongezea fursa za kiuchumi na kuongeza :" Tunawaelimisha wanawake wanahabari kuelimika kuhusu matumizi ya teknolojia na mtandao. Wakati matumizi ya teknolojia yakikua ipo haja ya kuwa makini na matumizi na wavamizi hasa wale wa kimtandao wanaoiba na kuvujisha siri za mteja," anasema Zaituni.

### IDADI YA WATUMIAJI

Zaituni anasema hivi sasa takwimu duniani zinaonyesha watumiaji wa intaneti wameongezeka Tanzania ikiwa na wateja milioni 23 na duniani kote ni bilioni 4.5 na kwamba wakati matumizi yakikua duniani ni muda wa kuongeza usalama kimtandao kwa mtumiaji na wadau kwa kuwawezesha namna ya kuweka usiri wa taarifa na data zao.

Akizungumzia changamoto Zaituni anasema baadhi ya taarifa zilizopo katika mtandao zina usalama mdogo, huku wanawake kadhaa wakiathiriwa zaidi kutokana na elimu ndogo ya matumizi ya huduma hizo akitaja changamoto kubwa kuwa ni uelewa mdogo kwa wanaotakiwa kufikisha habari kupitia mtandao, ili kutoa taarifa sahihi, kuelimisha umma kipindi ambacho dunia inahitaji kufahamu na elimu zaidi.

Zaituni anasema kutokana na watu wengi kuwa na elimu ndogo ya kulinda taarifa, picha zao imekuwa ni kawaida kuona picha za kudhalilisha hasa wanawake zikisambaa maeneo tofauti bila wao kujua na kwamba changamoto hiyo inawahusu hawa mabinti ambao wakati mwingine hudanganyika kwa urahisi kutumia au kupiga picha bila kufahamu athari zake.

Katika mafunzo hayo wanahabari wanaona kuwa yamewafungua macho. Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Zahara Tunda, anasema yamemwongezea uelewa wa kulinda mifumo yote ambayo inahusisha mtandao na kwamba katika kazi zake mara nyingi anategemea mtandao na kwamba amekuwa na uelewa zaidi wa namna ya kuimarisha shughuli zake.

Ibrahim Samatta anasema waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kupasha habari jamii, hivyo kupata mafunzo hayo ni kuongeza uelewa na haja ya kuwa na umakini zaidi katika kazi na kuomba elimu hiyo isambae kwa watetezi wa haki za binadamu, ili kuwaongezea uelewa zaidi katika masuala ya usalama wa mitandao.

Samatta anasema mafunzo ya usalama wa mitandao kwa wanahabari ambao watakuwa na jukumu kubwa la kutoa taarifa za uchaguzi na kuwa katika hali ya hatari na vyombo vyao vinaweza kudukuliwa na kuwataka washiriki wa mafunzo hayo wazingatie, elimu na kuifanyia kazi kikamilifu ili kuwaepusha na hatari za usalama wa kimtandao.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), katika chapisho la mwongozo wa matumizi ya huduma na bidhaa za mawasiliano, unasema miaka ya hivi karibuni kasi ya kukua kwa sekta ya mawasiliano hapa nchini na duniani imekuwa kubwa na kwamba kumekuwa na ongezeko la huduma zinazowezeshwa na Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na fursa zinazotokana na kuongezeka idadi ya watumiaji na watoa huduma.

Katika mwongozo huo unaelezea matumizi ya mitandao ya kijamii na masuala ya jumla ya intaneti, kwamba mitandao ya kijamii ambayo imewezeshwa na kuwapo kwa intaneti imechangia katika kubadilishana taarifa, kufungua fursa za kujiendeleza na kwamba umekuwa chombo cha kupata na kubadilishana elimu, masuala ya kijamii na pia kama chanzo cha kipato kwa wajasiriamali na wateja wa magazeti, kusikiliza redio na kutazama televisheni kazi inayofanywa kupitia mitandao ya kijamii.

Mwongozo unakumbusha kuwa unapotumia kifaa cha mawasiliano kupata intaneti na kuwezesha kupata huduma za intaneti, ikiwa ni pamoja na simu za kiganjani, yanatakiwa pia kuzingatia sheria na staha na pia kumhakikishia mtumiaji faragha. Mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Facebook, Twitter na Instagram na mingineyo inawezeshwa kupitia intaneti.

Kwamba mtumiaji wa intaneti anashauriwa kuzingatia kutokuweka taarifa nyingi za binafsi na za undani kwenye mitandao ya jamii, kuwa makini kwenye matumizi ya neno la siri , lakini pia kujiepusha na kuweka picha chafu kama za utupu, ngono na matendo mengine yanayoweza kumwingiza kwenye jinai mitandaoni.

Unafafanua kuwa na staha na heshima kwa wahusika wa taarifa zinazosambazwa, kwa mfano kutokusambaza taarifa ambazo zinatia simanzi na taharuki kama picha zinazoonyesha kwa karibu sura au miili ya waathirika wa ajali au majanga pamoja na picha au video za matukio ambayo yanachangia kuharibu maadili na kujenga misingi potofu kwa watoto.

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Ilani zinavyochagiza elimu bora vyuo vikuu




Mwenyekiti wa Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Derpha Mpata, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa ilani ya chama hicho. Wa pili kulia ni mgombea urais kupitia SAU, Muttamwega Mgaywa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

UPATIKANAJI wa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu na hata urejeshwaji wake ni sintofahamu.

Hali hiyo inasababisha usumbufu kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) na pia kwa wanufaika wakiwamo wanaodai kukosa mikopo hiyo na kuwasababishia usumbufu, lakini wahitimu wa vyuo wakiendelea kudaiwa na HESLB na kusababisha wasakwe.

Kwa ujumla kila upande una malalamiko yake kwenye elimu ya juu, ambayo hadi 2020 hayajapatiwa ufumbuzi wa kudumu, kwa kuwa bado yanaendelea.

Kwa mfano Januari mwaka jana, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul- Razaq Badru, anasema msako mkali utaanza kuwasaka wanufaika zaidi ya 109,980 ambao hawajaanza kurejesha Sh. bilioni 291.5 walizokopeshwa.

Utaratibu unataka wanufaika kupewa mikopo iwapo wametimiza vigezo, lakini wanapohitimu vyuo wanatakiwa kuirejesha ili itumiwe na wanafunzi wengine, tena wasingojee kusakwa.

Wakati hayo yakiendelea kati ya bodi na wasomi, baadhi ya vyama vya siasa vimekuja na kile ambacho vinaamini kuwa ni suluhisho la changamoto kwenye elimu ya juu.

Kila chama kimeandaa ilani ikiwa imesheheni matarajio mengi kwa Watanzania likiwamo suala la elimu ya juu na mikakati ya kuiboresha ili kuondoa changamoto mbalimbali kwa bodi na wanufaika.

> Ilani ya Chama cha Wananchi (CUF), inawaaminisha Watanzania kuwa hakuna haja ya wanafunzi wa elimu ya juu kuchangia gharama.

### ELIMU YA JUU BURE

Ilani ya Chama cha Wananchi (CUF), inawaaminisha Watanzania kuwa hakuna haja ya wanafunzi wa elimu ya juu kuchangia gharama.

Inaliona hilo kama jukumu la serikali na kwamba wakiingia madarakani wataweka utaratibu utakaowawezesha vijana wenye sifa na waliochaguliwa kujiunga katika chuo kikuu chochote ndani ya nchi wanapata elimu ya juu bila vikwazo.

Aidha, serikali ya umoja wa kitaifa ya CUF, itagharamia mahitaji yote ya msingi ya mwanafunzi wa elimu ya juu bila mkopo, ikiwa ni pamoja na kugharamia bima ya afya ya kila mwanafunzi. Kuboresha eneo hili la elimu ya juu kutafanyika hatua kwa hatua, kwa kuzingatia hali halisi ya kukua kwa uchumi na mahitaji mengine ya taifa.

Ilani inasema serikali yao, itahakikisha wanafunzi wa elimu ya juu wanapatiwa posho zinazokidhi mahitaji wanapokuwa vyuoni katika mafunzo kwa vitendo.

### KUIMARISHA MFUMO

Ndani ya Ilani ya CCM, kuanzia ukurasa wa 127, kifungu (h), kinasema, serikali ya chama hicho, itaimarisha na kuboresha mfumo wa kugharamia elimu ya juu.

Ilani hiyo inagusa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wenye sifa stahiki wanapata fursa ya kujiunga na elimu ya juu.

Katika ukurasa wa 129 hadi 130, kifungu (f) ilani hiyo inazungumzia kuongeza udahili katika elimu ya juu kwa makundi yote yakiwamo ya wanafunzi kutoka nje ya nchi.

Ndani ya kifungu (g), CCM inasema, itaimarisha mfumo wa malezi kwa wanafunzi vyuoni kwa kuwapa stadi za maisha na huduma za ushauri nasaha ili kupata wahitimu wenye maadili.

### MAREJESHO MKOPO

Sehemu ya 5.5.2 ya ilani ya CHADEMA, ndani ya ukurasa wa 34, inasema kuundwa kwa bodi hiyo ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, hakujasaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo.

Inasema, kundi kubwa la wahitimu wa kidato cha sita wenye sifa limekuwa likikosa mikopo ya kuendelea na masomo. Hata hivyo, vigezo vya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi hauzingatii hali halisi ya maisha na uwezo wa kifedha wa wazazi wa wanafunzi.

Inasema jukumu la kugharamia elimu ya juu ndiyo changamoto kubwa kwenye sekta ya elimu, hivyo kusababisha watu wenye sifa za kusoma kushindwa kupata ufadhili wa serikali.

Ilani hiyo inafafanua kuwa, kwa muktadha huo, serikali ya chama hicho itahakikisha wale wote wenye sifa za kujiunga na vyuo vya kati, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu wanapewa mikopo bila ya ubaguzi.

CHADEMA inasema, fedha hizo ni za mikopo na si bure, hivyo serikali yao itapunguza kiwango cha marejesho ya mikopo hadi kufikia asilimia tatu ya mshahara wa mnufaika na kutanua wigo wa muda wa marejesho hadi kufikia miaka 25 tangu mnufaika apate ajira.

Serikali yao itafuta riba na tozo zote zitokanazo na adhabu ya kuchelewesha marejesho ya mkopo wa elimu ya juu. Lengo kuu la kupunguza kiwango cha marejesho na kuongeza muda wa kulipa ni kuweka mazingira wezeshi ili kila mhusika alipe na usiwe mzigo wa kumfanya asiweze kuwekeza katika shughuli zingine za uzalishaji.

### MIKOPO KUFUTWA

Chama cha ACT-Wazalendo katika ilani yake kinaahidi kufuta mikopo yote ya wahitimu watakaoingia mikataba maalum na serikali ya kufanya kazi kwa miaka mitatu mfululizo katika maeneo ya pembezoni na yenye mazingira magumu ya kazi, kwa zile sekta mahsusi kama utabibu, ualimu, maofisa ugani kwa kilimo, ufugaji na uvuvi.

Aidha, kitatunga sheria kuhakikisha kuwa mikopo ya elimu ya juu inakuwa ni kwa ajili ya kugharamia chakula na malazi.

Chama hicho kinakusudia pia kughamia mafunzo kwa vitendo kwa fani zote kwa kipindi kisichopungua miezi sita ili wanafunzi wote wapitie mafunzo hayo kikamilifu.

Vilevile kinaahidi kuweka utaratibu wa kutumia matokeo ya mafunzo kwa vitendo katika utoaji ajira, ili kuhimiza wanafunzi kuona umuhimu wa mafunzo kwa vitendo.

### KUDHIBITI NGONO

Mbali na hayo, chama hicho kinaahidi kuwa vyuo vikuu vyote vinaweka sheria na taratibu mahususi kuzuia rushwa ya ngono, huku vyuo vikuu vyote vikiwa na programu maalum inayolenga kutengeneza mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu kupata elimu ya juu katika fani walizochagua kwa urahisi na ufanisi.

### WOTE KUINGIA CHUO KIKUU

Chama cha Sauti ya Umma (SAU), katika ilani yake kinaamini kwamba, elimu bora ndiyo msingi wa maendeleo ya taifa hili, hivyo kinakusudia kuwekeza zaidi katika elimu bora.

Lengo kuu ni kupata wataalamu bora watakaoshiriki kukamilisha mipango mbalimbali ya maendeleo ya taifa, lakini kikubwa zaidi kinataka kila Mtanzania afikie elimu ya chuo bila malipo.

Elimu hiyo inayotajwa na chama hicho ni ya vyuo vya ufundi stadi, mafundi mchundo hadi chuo kikuu, kwa lengo la kusaidia kupata wataalamu wengi zaidi wa fani mbalimbali.

Hayo yamo ndani ya ukurasa wa 11 wa ilani ya chama hicho ikifafanua kuwa lengo ni kila Mtanzania kwa uwezo wa elimu yake achangie pato la taifa kwa kuajiriwa ama kujiajiri.

SAU katika ilani hiyo inasema, itahakikisha maslahi ya walimu yanazingatiwa, wanapata huku wakiwa katika mazingira bora ya kufundishia wakiwa na vitendea kazi kama vitabu, vifaa vya maabara na kemikali.



# Walimu wahimizwa kupiga kura

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimewahimiza walimu kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu, ili kuchagua viongozi bora.

Aidha, chama hicho ndani ya miezi mitatu (Julai-Septemba, 2020) kimelipa zaidi ya Sh. milioni 600 kwa wastaafu 1,775 kama mkono wa kwaheri.

**Tunaendelea kusisitiza walimu kujiunga na CWT tunahitaji kuona uchaguzi huu walimu wanashiriki kwa wingi ili kupata viongozi bora.**

Akifunga semina ya siku mbili iliyofanyika jana wilayani Kondoa na kujumuisha walimu kutoka mikoa ya Kanda ya Kati, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema walimu hao wajitokeze kushiriki ipasavyo kwenye uchaguzi huo ili kupata viongozi watakaoongoza kwa miaka mingine mitano ijayo.

"Tunaendelea kusisitiza walimu kujiunga na CWT tunahitaji kuona uchaguzi huu walimu wanashiriki kwa wingi ili kupata viongozi bora," alisema Seif.

Naye Makamu wa Rais wa CWT, Dinah Mathaman, alisema CWT itaendelea kusaidiana na serikali kuwahudumia walimu kwa ukaribu na ufanisi ili kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili.

Mathaman alisema wao kama viongozi kwa umoja wao wamejipanga kuwatetea na kulinda maslahi ya walimu kwa weledi ili kuhakikisha walimu wanakuwa salama. Alisema kwa muda mfupi uongozi wao wamekutana na viongozi mbalimbali wa serikali wanaohusika na masuala ya walimu kujadiliana namna bora ya kutatua kero hizo na baadhi zimeanza kutatuliwa ikiwamo ajira za walimu, ulipwaji wa malimbikizo ya mishahara na ulipwaji wa madeni yasiyo ya mishahara.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa CWT, Japhet Maganga, aliwaasa wanachama kuendelea kuuamini uongozi uliopo madarakani.

Aliwataka kuwa waadilifu kwenye usimamizi wa mitihani ya taifa inayotarajiwa kuanza mapema Oktoba, 2020.

## Mwalimu mkuu mbaroni tuhuma za rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, inamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Karume Wilaya ya Kongwa, Mwakangale Mwasikila, kwa tuhuma za kushawishi kupokea rushwa ili atoe cheti cha kuhitimu darasa la saba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkuu wa Taasisi hiyo mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, alisema mwalimu huyo alishawishi kupokea rushwa ya Sh. 55,000 ili atoe cheti hicho kwa kijana ambaye alihitaji atumie cheti hiko kuomba nafasi ya kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Kibwengo alisema katika uchunguzi wao wamebaini mwalimu huyo alishatoa vyeti vingi kwa watu ambao sio sahihi na hawakusoma katika shule hiyo. Katika hatua nyingine, taasisi hiyo imesaidia wakazi wa Kelema Kuu wilayani Chemba, kupata maji baada ya kukosa takribani miaka mitano, kutokana na mradi wa maji kutekelezwa chini ya kiwango.

Kibwengo alisema taasisi hiyo ilipokea taarifa kuhusu mradi huo, ambao ulikuwa unatekelezwa na Kampuni ya Juan na ilianza uchunguzi ambao ulibaini kuwapo kwa viashiria vya rushwa ambavyo vilisababisha mkandarasi wa awali kutandika mabomba ambayo hayana uwezo wa kusukuma maji kupanda katika tangi.

"Baada ya kugundua hilo mkandarasi aliamriwa kurejesha kiasi cha fedha zaidi ya Sh. milioni 15 pamoja na kutandika mabomba mengine yenye uwezo wa kusukuma maji," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kutekeleza hilo hivi sasa wakazi takriban 3,500 wanapata maji katika vituo vitano bila msongamano wowote.

Aidha, alisema mkandarasi huyo ametakiwa kuhakikisha maji hayo yanatoka ili wananchi wasipate kero yoyote na kwamba wataendelea kufuatilia mradi huo kuhakikisha hakuna hujuma itakayofanyika kuzuia maji yasitoke.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Kelema Kuu, Kirwa Kibunde, alishukuru TAKUKURU kwa kusimamia mradi huo ambapo awali wakazi hao walikuwa wakifuata majisafi na salama kwa umbali mrefu.

"Tunawashukuru sana TAKUKURU kwa kutusaidia kupata maji wanawake walikuwa hawakai nyumbani kutwa kucha kutembea kutafuta maji," alisema Kibunde.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Mary Maganga (kulia), akikabidhi taarifa ya mpango mkuu wa miaka 10 wa maendeleo ya sekta ya fedha nchini kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Hisham Hendi kwa niaba ya watoa huduma za mawasiliano, baada ya mpango huo kuzinduliwa rasmi jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madoga wa CHADEMA kuipaisha Dodoma kwa huduma za jamii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Aisha Madoga, amesema akichaguliwa atahakikisha anaboresha sekta ya elimu, afya pamoja na maji.

Madoga, aliyasema hao juzi jijini hapa kwenye uzinduzi wa kampeni zake uliofanyika Kata ya Chang'ombe.

Alisema, akichaguliwa ataipa kipaumbele sekta ya elimu ili watoto wapate elimu bora na siyo bora elimu.

Alisema, hivi sasa elimu nchini inakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo uhaba wa madawati, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, uhaba wa walimu hasa katika masomo ya sayansi pamoja na matundu ya vyoo.

"Mimi nikiwa mbunge wa jimbo hili nitahakikisha kuwa hizo kero zote tunazifanyia kazi ili watoto wetu wasome katika mazingira mazuri na yatakayo wawezesha kujifunza katika mazingira rafiki kuliko sasa," alisema.

Vile vile, alisema kuwa kutokana na elimu kuwa ufunguo wa maisha, yeye kama mwakilishi wa wananchi atahakikisha kuwa maeneo yote yenye kero anayafanyia kazi katika kipindi chake cha ubunge na kubaki historia.

Pia, Madoga alisema kuwa kero nyingine atakayoifanyia kazi ni sekta ya maji ambapo atahakikisha kuwa anaishughulikia kwa kuboresha miundombinu ya huduma za maji ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima hasa katika maeneo ya vijijini.

"Hivi sasa maji imekuwa ni kero kubwa sana hasa katika maeneo ya vijijini mimi nikiwa mbunge nitahakikisha kwa kushirikiana na wadau wengine huduma za maji zinaboreshwa ili kuwasaidia kinamama ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu kila siku," alisema Madoga.

Aidha, alisema atahakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za matibabu bora katika maeneo wanayoishi na kuondoa adha ya kutembea umbali mrefu kufuata matibabu.

"Sekta ya afya ndiyo msingi wa maendeleo, mtu bila kuwa na afya bora hawezi kushiriki hata katika shughuli za maendeleo, hivyo basi mimi nitahakikisha kuwa suala la sekta ya afya linakuwa kipaumbele chake," alisema Madoga.

Chama hicho kimezindua rasmi kampeni zake za ubunge jijini Dodoma, baada ya mgombea wake wa ubunge kurejeshwa na Tume ya Taifa ya uchaguzi (NEC) baada ya rufani yake kukubaliwa.



# Chupa za damu 500 kukusanywa siku saba Nyanda za Juu Kusini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHUPA 500 zinatarajiwa kukusanywa na benki ya damu salama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizopo Hospitali ya Wazazi Meta mkoani Mbeya, huku chupa 100 za damu ambazo ni sawa na uniti 500 zinatarajiwa kukusanywa kila siku katika wiki ya uchangiaji damu.

Wiki ya uchangiaji damu ilianza jana Septemba 21 hadi 25 mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo cha kuchangia damu Nyanda za Juu Kusini, Bahati Tembo, aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Wiki la Uchangiaji Damu, ambapo alisema wanalenga kuokoa maisha ya mama na mtoto, majeruhi wa ajali pamoja na wagonjwa wengine wenye mahitaji ya damu.

Bahati alisema wiki ya uchangiaji damu mwaka huu iwameamua kulifikia kundi la askari mgambo kwa sababu lina watu wengi na wanafikika kirahisi na kwamba wamefikia umri wa kuanzia miaka 18 ambayo ni sifa mojawapo inayohitajika katika kuchangia damu.

**Mwaka huu katika Wiki ya Uchangiaji Damu tumeamua kuwafikia askari mgambo kwa sababu ni kundi ambalo linajitolea kwenye masuala mbalimbali, tutafika kila makambi ya askari mgambo ili kukusanya damu kwa wingi ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu.**

"Mwaka huu katika Wiki ya Uchangiaji Damu tumeamua kuwafikia askari mgambo kwa sababu ni kundi ambalo linajitolea kwenye masuala mbalimbali, tutafika kila makambi ya askari mgambo ili kukusanya damu kwa wingi ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu," alisema Tembo.

Aliongeza kuwa kwa Mkoa wa Mbeya jumla ya askari mgambo 1,000 wanatarajiwa kuchangia damu, na kwamba kwa siku watahakikisha wanakusanya uniti 500 ambazo ni sawa na chupa 100 za damu katika kila wilaya watakayofika.

Akizungumzia mwitikio wa wananchi kuchangia damu, alisema ni mdogo na kwamba wananchi wa Mkoa wa Mbeya ni wabishi kushiriki zoezi hilo licha ya kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuchangia damu.

Aliongeza kuwa mwaka huu hawawezi kulifikia kundi la wanafunzi hususani wa sekondari kwa sababu wengi wao wanajiandaa na mitihani, lakini asilimia kubwa ya wanafunzi hawajafikia umri wa miaka 18 ukilinganisha na askari mgambo ambao wengi wamevuka umri huo.

Mmoja wa askari mgambo ambao walishiriki zoezi la kuchangia damu, Charles Mgogo kutoa eneo la Sabasaba, alisema aliamua kuchangia damu kwa sababu ya kuokoa maisha ya mama na mtoto na kwamba utayari huo unaweza kuwa fadhila na kwake atakapopata matatizo.

Aliwahamasisha wananchi kuendelea kuchangia damu kwa madai kuwa mahitaji bado ni makubwa na wataoweza kuokoa maisha ya wenzao ni wale ambao wanasifa ya kuchangia.

Mustafa Mgweno, alisema yeye ni mara ya kwanza kuchangia damu na alishawishika kufanya hivyo baada ya kupewa elimu juu ya faida za kuchangia damu kutoka kwa wataalamu wa kitengo hicho walipowatembelea.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wenye Ulemavu Kitengo cha Damu Salama, mwaka 2020 kimelenga kukusanya chupa 32,700 huku timu za mikoa ni chupa 150, timu za damu salama vituo vya kanda chupa 500 Hospitali za Kanda chupa 150.



Mtaalamu wa Mishipa kutoka Kitengo cha Damu Salama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Aloyce Fabian, akiwahudumia mgambo walioshiriki zoezi la uchangiaji damu lililoandaliwa na kitengo hicho, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wafugaji nyuki wapewa mbinu kuepuka umaskini

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

VIKUNDI vitano vya wafugaji wa nyuki katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe vimepatiwa mafunzo ya namna bora ya ufugaji, mizinga na soko ili waweze kujikwamua na umaskini.

Kampuni ya uchimbaji wa madini ya Shanta Gold Mine (New Luika) ndio iliyovisaidia vikundi hivyo kuwapatia mizinga, mafunzo na soko baada ya kuona hawanufaiki na ufugaji wa nyuki.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa vikundi hivyo, Kaimu Meneja wa Shanta Gold Mine (New Luika), Exupery Lyimo, alisema kampuni hiyo iliviwezesha vikundi hivyo, ili sasa waanze kupata faida na kuweza kujikwamua na umaskini kutoka maeneo ya Saza na Mbangala.

Alisema kampuni hiyo ilianza kuviwezesha vikundi hivyo mwaka 2017 kwa kuanza kuvipa mizinga ya nyuki na kwamba kampuni yenyewe ndio mnunuaji wa asali ambazo zinazalishwa na vikundi hivyo.

Lyimo alisema baada ya kuanzisha vikundi hivyo kampuni ya Shanta ilitoa jumla ya mizinga 250 kwa vikundi hivyo katika maeneo ya Saza na Mbangala pamoja na mashine 10 zinazotumika kuvuna asali.

"Mkuu wa Wilaya ya Songwe, alitufuata sisi wadau wa maendeleo ili tuone ni kwa namna gani tunashirikiana na jamii katika eneo la ufugaji nyuki, pamoja na kutoa mizinga hiyo, pia tuliwaleta wataalamu wa nyuki kutoka Tabora kwa ajili ya kutoa elimu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samwel Jeremiah, alizitaka taasisi za kifedha wilayani humo kupunguza masharti ya kukopa ili vikundi hivyo vinufaike na mikopo bila kuumia.

"Ufugaji wa nyuki ni fursa, hivyo nawasihi wafugaji mzingatie elimu mliyopewa ili mfuge kisasa na kupata faida kwa sababu mmehakikishiwa soko na kampuni hii," alisema Jeremiah.

# Rai kuwafichua watoto wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JAMII imeshauri kuwafichua na kuwapeleka kwenye ofisi za ustawi wa jamii watoto wenye ulemavu ambao wanafichwa na wazazi au walezi wao, ili wapatiwe haki zao za msingi ikiwamo elimu, chakula na malazi.

Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Kyela, Paul Mabula, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari vijana ambao ni wanufaika na Mradi wa Sauti Mpya kutoka mkoani Mbeya.

Alisema watoto wenye ulemavu hukosa haki zao za msingi kwa sababu ya jamii kutozifahamu sheria ambazo zinaelekeza kundi hilo la watoto kupata huduma hata kwenye ofisi za Ustawi wa Jamii. Alisema maofisa Ustawi wa Jamii wanapaswa kutoa elimu kwa wananchi kufika katika ofisi zao kwa lengo la kuwapatia misaada kwa sababu serikali ilielekeza huduma hizo zitolewe pale inapobidi kutokana na mazingira husika.

"Jamii inapaswa kufahamu kuwa watoto waliofichwa aidha na wazazi au walezi wana haki ya kupata huduma zote za msingi na kama familia ni maskini basi jukumu la kuhudumia litakuwa ni la maofisa ustawi wa jamii kwa sababu serikali iliekeleza na nina imani bajeti ipo," alisema Mabula.

Aliongeza kuwa katika Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kifungu cha 8 (v) hadi cha (vi) kimeelekeza wajibu wa ofisa ustawi wa jamii jukumu la kumhudumia mtoto mwenye ulemavu ambaye kwa namna moja au nyingine familia imemtelekeza au haina uwezo wa kumpatia mahitaji yake.

Vilevile, aliwaomba wanahabari kupitia kalamu zao kuelimisha jamii kutowaficha watoto ndani badala yake wawafichue ili waweze kupata misaada kutoka kwa wadau mbalimbali yakiwamo mashirika ya binafsi na serikali.

Aidha, aliiomba jamii pamoja na familia ambazo zina watoto wenye ulemavu kulisaidia kundi hilo katika kutimiza ndoto zao ikiwamo kupatia elimu, chakula na malazi.

Baadhi ya wanahabari walishiriki mafunzo hayo akiwamo Baraka Mwambungu alikiri kuwa elimu hiyo ya watoto wenye ulemavu wanapaswa kuhudumiwa na maofisa ustawi wa jamii kutokana na sababu mbalimbali kama vifo kwa wazazi au walezi, umaskini na vificho kwa watoto hao haikuwapo hivyo elimu hiyo itasaidia kuongeza uelewa.





# Mgombea urais CUF ajinadi kujenga vyuo vikuu Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Mussa Haji Kombo, amesema iwapo wananchi watamchagua kuwa Rais wa Zanzibar ataimarisha sekta ya elimu na kuanzisha vyuo vikuu kisiwani Pemba.

Aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kampeni za chama hicho zilizofanyika Viwanja vya Tibirinzi Kisiwani Pemba.

Aliwataka wananchi kisiwani humo kuachana na ubaguzi na kuwa wamoja ili Zanzibar iweze kupata maendeleo na kumpigia kura katika uchaguzi mkuu ambazo zitamwezesha kupata ushindi.

Naye mgombea urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia chama hicho, Profesa Ibrahim Lipumba alisema chama hicho kitaendelea kusimamia sera yake ya haki sawa kwa wananchi wote.

Alieleza kuwa katika jambo ambalo CUF walifanikiwa ni mabadiliko ya katiba inayozungumzia uwapo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Mgombea huyo aliwasihi wananchi kutokuwa tayari kusikiliza kauli za uchochezi zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa ambazo zinaweza kupelekea fujo na machafuko.

Aidha, Profesa Lipumba aliziomba tume za uchaguzi kutenda haki kwa vyama vyote ili kufanya uchaguzi huru na haki.

**Mgombea huyo aliwasihi wananchi kutokuwa tayari kusikiliza kauli za uchochezi zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa ambazo zinaweza kupelekea fujo na machafuko.**

# Mwinyi kuifanyia maboresho Sheria ya Magazeti ya 1988

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa endapo atapata ridhaa ya Wazanzibari kuwa rais wa Zanzibar, atahakikisha anaifanyia maboresho Sheria ya Magazeti ya Zanzibar ya Mwaka 1988, kutokana na kupitwa na wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, alisema kuwa kufanyiwa kwa marekebisho kwa sheria hiyo kutatoa uhuru kwa vyombo vya habari.

Alisema kupitia sheria hiyo atahakikisha anaboresha maslahi na ulinzi kwa waandishi wa habari Zanzibar, ili kufanya kazi zao kwa uweledi bila ya kubugudhiwa.

Alieleza kuwa anafahamu kuna urasimu mkubwa wa kupata habari, hivyo atakapoingia madarakani atahakikisha anaondoa urasimu huo na kiongozi yoyote atakayekataa kutoa habari kwa waandishi wa habari atamwajibisha.

**Nafahamu kuwa hivi sasa waandishi wa habari hasa wa vyombo binafsi mna wakati mgumu wa kujiendeleza kielimu, hivyo nitahakikisha mnaendelea kupata elimu huku mkiwa kazini.**

Aidha, alisema atahakikisha Zanzibar ina sheria ambayo itatetea maslahi ya waandishi wa habari ikiwamo wamiliki wote wa vyombo vya habari kwa kushirikiana na serikali inawaendeleza waandishi wao kielimu wakati akiwa kazini.

"Nafahamu kuwa hivi sasa waandishi wa habari hasa wa vyombo binafsi mna wakati mgumu wa kujiendeleza kielimu, hivyo nitahakikisha mnaendelea kupata elimu huku mkiwa kazini," alisema Dk. Mwinyi.

Alieleza kuwa fursa ya kujiendeleza kielimu kwa waandishi wa habari wakiwa bado wapo kazini ipo kwa waandishi wa habari wa vyombo vya serikali, lakini kwa vyombo binfasi ni vigumu, hivyo mwandishi analazimika kuacha kazi ndio ajiendeleze bila ya kuwapo kazini.

Mgombea huyo aliwataka waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa kufuata maadili ya taaluma yao na kutojihusisha kuandika au kuchapisha machapisho ambayo yataashiria uvunjifu wa amani.

"Kalamu ya mwandishi wa habari ni moja ya nyenzo muhimu ikiitumika vizuri, lakini kalamu hiyo hiyo inaweza kubomoa zaidi kuliko upanga au silaha na kusababisha machafuko makubwa na ndicho kilichofanyika Burundi na nchi zingine zenye machafuko," alisema.

Hata hivyo, mgombea huyo aliwataka waandishi wa habari kuihabarisha jamii kuhusu kuhubiri na kuilinda amani ya nchi iliyopo hasa katika kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi mkuu.



Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utafiti wa Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar, Daima Mkalimoto (kushoto), akizungumza katika mkutano wa kufunga mradi wa kukuza upatikanaji wa haki kwa wanawake, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara ya Katiba yajipanga kuzitatua kero sugu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Sera, Mipango na Utafiti wa Wizara ya Katiba na Sheria, Daima Mkalimoto, amesema migororo ya ardhi, watoto wa kike kutokushirikishwa katika mirathi na watoto kukosa matunzo baada ya wanandoa kuachana ni miongoni mwa changamoto kubwa ambazo zinaikabili jamii.

Aliyasema hayo katika hafla ya kufunga mradi wa kukuza upatikanaji wa haki kwa wanawake kupitia wasaidizi wa sheria, uliokuwa ukifanywa kwa pamoja na wasaidizi wa Sheria na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) chini ya ufadhili wa shirika linalosaidia upatikanaji wa huduma za kisheria (LSF), iliyofanyika ukumbi wa studio ya filamu Rahaleo mjini Unguja.

Alisema juhudi za makusudi zinahitajika kuchukuliwa katika kuhakikisha masuala hayo yanapatiwa ufumbuzi kwa haraka.

"Ni faraja kubwa sana kuona kwamba wasaidizi wa sheria wanafanyakazi nzuri ya kusaidia jamii katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kisheria ikiwamo kutatua migogoro ya ardhi hasa kwa kutumia njia mbadala za usuluhishi bila kuihusisha mahakama," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wasaidizi wa sheria kuendelea kuwasaidia wananchi kutambua haki zao za kisheria na kuweza kuzifuata.

Alisema upatikanaji wa haki ni nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umaskini nchini.

Alisema suala la msaada wa kisheria limetamkwa bayana katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar (MKUZA), kwa kuwa na kaulimbiu hiyo ya upatikanaji wa haki ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya nchi ambayo inapaswa kuheshimiwa na kuendelezwa.

Mkalimoto alisema wakati wanaandaa sera ya msaada wa kisheria ilibainika kuwa ipo changamoto ya idadi ndogo ya watoa huduma za msaada wa kisheria ambayo haiwezi kukidhi mahitaji ya wananchi.

Alieleza kuwa ni fursa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria kujisajili na kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, ili kufanikisha azma ya serikali ya kuwafikia wote wenye kuhitaji huduma za sheria na msaada wa kisheria.

Kadhalika, alisema kwa kuwa serikali imeainisha serikali za mitaa ili kuwasogezea wananchi huduma karibu zaidi, asasi kama Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na wasaidizi wa sheria wanayofursa kufanya kazi na mamlaka husika zilizopo katika maeneo yao.

Akisoma risala ya wanajumuiya ya wasaidizi sheria, Bikubwa Haji Kheri, alisema kupitia mradi huo ambao unashirikisha wilaya tatu za Unguja ikiwamo Wilaya ya Kati, Kusini na Magharibi 'B', wamepata fursa kubwa ya kujifunza mambo mbalimbali ambayo ni changamoto kwa wananchi wa maeneo hayo na kuwapa miongozo ya kutatua changamoto hizo.

Aidha, alisema jumuiya hizo zimeshafikishiwa mashauri, manung'uniko na kesi nyingi ambazo kati ya hizo kesi, 184 ni za uzalilishaji ambapo 32 zinawahusu wanaume na 152 wanawake.

Alisema kuna kesi 160 zinaendelea katika taasisi zao ambazo kati ya hizo 47 ni za watoto wa kiume na 111 zinawahusu wanawake na kesi 43 wamezipatia rufani katika taasisi mbalimbali kwa kupatiwa ufumbuzi zaidi.

Mkurugenzi wa ZAFELA, Jamila Mahmoud, alisema mradi huo umesaidia kutambulika na kuaminiwa kwa wasaidizi wa sheria katika jamii.

## HABARI KIMATAIFA

## Upinzani Ivory Coast wapinga rais kuwania muhula 3

**YAMOUSSOUKRO,** Ivory Coast

WAPINZANI wakuu wa uchaguzi wa urais nchini Ivory Coast, wamewataka raia kuandamana, ili kumzuia Rais Alassane Ouattara, kuwania muhula wa tatu wa nafasi ya urais katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Henri Konan Bédié rais wa zamani wa taifa hilo, alitangaza kuwa vyama vya upinzani viliungana ili kulinda amani.

Takribani watu 10 wameuawa tangu ghasia zianze mwezi uliopita, baada ya Ouattara kutangaza kuwania tena nafasi ya urais baada ya mrithi aliyechaguliwa kufariki ghafla.

Uchaguzi huo unaonekana kuwa mtihani mkubwa wa kulinda amani ya mataifa ya Afrika Magharibi, tangu mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yaliosababishwa na uchaguzi, miaka 10 iliyopita. **BBC**

## Vital Kamerhe asikiliza kesi yake

**KINSHASA,** DRC

MSHIRIKA mkuu wa serikali ya Rais Felix Tshisekedi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Vital Kamerhe, alitarajiwa kufika mahakamani jana, baada ya kushindwa kuhudhuria Ijumaa kutokana na sababu za kiafya.

Kamerhe alihukumiwa kifungo cha miaka 20 kwa kosa la ufisadi na wizi wa takriban dola milioni 50 za Marekani.

Aidha, Kamerhe hatoruhusiwa kuwania wadhifa wowote kwa miaka 10, baada ya kuhudumia hukumu yake na hata kushikilia wadhfa wowote wa serikali.

Kamerhe ndiye aliyesababisha Tshisekedi, awe Rais wa DRC. **BBC**

## Msaada UN Darfur baada ya miaka 10

**DARFUR,** Sudan

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), limepeleka misaada katika eneo la Jebel Marra, Darfur, Sudan ili kuokoa maisha ya watu waliokimbilia katika maeneo ya milima kukimbia mapigano katika maeneo yao.

Ngamia waliobeba misaada mbalimbali kutoka shirika hilo, walikatiza katika mabonde na vilima vya mawe.

Mkuu wa Ofisi ya UNICEF, Antony Spalton, alisema walipeleka vifaa vya muhimu kwa ajili ya shule, kliniki, dawa na mahitaji mengine ya kuokoa maisha vikiwamo vifaa vya kupima usalama wa maji na pia dawa ya kutibu maji.

Hii ni mara ya kwanza katika miaka 10, watoa misaada ya kibinadamu kuzifikia jamii hizo zilizotawanywa na mgogoro Kusini mwa Jebel Marra, Darfur, Sudan. **UN**

# Uganda kufungua shule, vyuo Oktoba

**KAMPALA,** Uganda

**Virusi vipya vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, viligunduliwa mwaka jana, Wuhan, China.**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametangaza kuwa shule na taasisi zingine za elimu ya juu, zitafunguliwa tena kuanzia mwezi ujao.

Hatua hiyo inakuja wakati Uganda kufikia sasa ikiwa imerekodi visa 5,380 vya maambukizi ya virusi vya corona.

Hata hivyo, wanafunzi milioni 1.2 walioko kwenye madarasa ya mwisho ya kufanya mitihani, ndio watakaoruhusiwa kurejea tena shuleni, baada ya serikali nchini humo kulegeza zaidi ya masharti ya kupambana na janga la corona.

Museveni alisema wanafunzi hao, watarejea shuleni kuanzia Oktoba 15, mwaka huu, na mikakati imewekwa kuhakikisha kuwa wanakuwa salama.

Shule zilifungwa nchini humo Machi mwaka huu, baada ya kuzuka kwa janga hilo ambalo limewaambukiza watu 6,287 na wengine 63 kupoteza maisha.

Virusi vya corona ni jamii kubwa ya virusi vinavyojulikana kusababisha magonjwa yanayoanzia homa ya kawaida hadi homa kali kama vile homa kali ya upumuaji ya Mashariki ya Kati (MERS) na homa kali ya mfumo wa upumuaji (SARS).

Virusi vipya vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, viligunduliwa mwaka jana, Wuhan, China.

Uganda, ilitangaza kifo cha kwanza kinachohusiana na COVID-19, Julai 23. mwaka huu.

Halmashauri ya Manispaa ya Jiji la Kampala ilianza kusambaza barakoa katika vitongoji vya jiji hilo.

Mamlaka pia iliongeza kampeni za kuwahimiza wananchi kupambana dhidi ya corona.

Mwishoni mwa mwezi Julai, Rais Museveni alitangaza kulegeza sehemu ya hatua zilizochukuliwa kudhibiti janga hilo, kurejesha hali ya kawaida kwa kufungua baadhi ya biashara, kulegeza sheria ya kutotoka nje na kuwaruhusu waendesha pikipiki za kukodiwa kufanya tena shughuli yao. **RFI**



Wakazi wa Kijiji cha Jawa, Jebel Marra Mashariki mwa Jimbo la Darfur Sudan ambao wamefikiwa na misaada iliyopelekwa na Umoja wa Mataifa (UN), ili kuokoa maisha ya watu waliokimbilia katika maeneo ya milima kukwepa mapigano katika maeneo yao. **PICHA: UN**

# Iran kuijibu Marekani baada ya vikwazo

**TEHRAN,** Iran

RAIS wa Iran Hassan Rouhani amesema Marekani "imeshindwa" katika juhudi zake za kuiwekea tena vikwazo nchi hiyo, baada ya washirika wake wa Ulaya kusema hatua hiyo haiambatani na msingi wa kisheria.

Katika hotuba iliyopeperushwa kupitia televisheni, Rouhani alisema Iran "itajibu vikali uonevu wa Marekani".

Utawala wa Marekani umesema vikwazo hivyo vinarejeshwa tena chini ya mkataba wa nyuklia ambao Marekani ilijiondoa.

Uingereza, Ufaransa na Ujerumani zimesema hazina uwezo wa kutekeleza hatua kama hiyo.

Nchi hizo tatu, pamoja China, Urusi na Marekani, zilitia saini mkataba mwaka 2015 kudhibiti mpango wa nyuklia wa Iran.

Lakini Rais Donald Trump, mkosoaji wa mkataba huo ulioafikiwa wakati wa utawala wa Obama, aliiondoa Marekani kwenye makataba huo mwaka 2018.

Kutokana na hilo, Iran ilianza kukiuka baadhi ya ahadi ilizotoa ikiwa ni pamoja na urutubishaji wa madini ya uranium zaidi ya kiwango kilichowekwa.

Siku ya Jumamosi, ofisa wa ngazi ya juu wa Marekani ambaye jina lake halikutajwa aliiambia shirika la habari la Reuters kwamba, kuanzia jana, Washington huenda ikaanza kuwawekea vikwazo baadhi ya watu na mashirika yatakayojihusisha na zana za nyuklia za Iran, makombora na mpango wake wa uundaji silaha ndogo ndogo. **BBC**

# DILI LA SUAREZ JUVE LAYEYUKA




**TURIN,** Italia

MKURUGENZI wa soka wa Juventus, Fabio Paratici, amethibitisha nyota wa Barcelona, Luis Suarez hatajiunga na mabingwa hao wa Serie A, huku akisisitiza klabu hiyo hamfikirii straika wa Roma, Edin Dzeko.

Ripoti za nchini Hispania zimebainisha miamba hao wa LaLiga, Barca wamemwambia mkongwe Suarez anaweza kuondoka na amekuwa akihusishwa kuungana na Cristiano Ronaldo kule Juve, baada ya kuondoka kwa Gonzalo Higuain aliyetua timu ya David Beckham, Inter Miami kwenye Ligi Kuu Marekani, (MLS).

Lakini kwa kushindwa kupata pasi ya kusafiria ya Italia, nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 33 sasa mipango hiyo imesitishwa, huku Paratici akithibitisha kabla ya mchezo wao wa ufunguzi wa Ligi Kuu England wa ushindi wa 3-0 dhidi ya Sampdoria, Jumapili.

"Suarez anaweza kuondolewa kwenye orodha hiyo, kwa sababu muda uliobaki ni mfupi mno kumwezesha yeye kupata hati ya kusafiria ya Italia au muda wa kumweka kwenye kikosi cha Ligi ya Mabingwa Ulaya," amesema Paratici.

"Tumetathmini hali halisi ya Suarez, tumeona kwamba itamchukua muda kupata uraia wa Italia, hivyo tumeachana na mpango wa kumchukua.

"Haiwezekani kwa sasa, na wala hakukaribia kutua hapa."

Huku Suarez akiondolewa kwenye orodha hiyo, kocha mpya wa Juve, Andrea Pirlo – ameendelea kuhusishwa na nyota wa Roma, Dzeko.

Lakini Paratici amebainisha kwa sasa wanahitaji mshambuliaji wa kati kuwasaidia Cristiano Ronaldo na Paulo Dybala, lakini sio majina yanayotajwa.

# Klopp asifia kiwango cha Fabinho




**LONDON,** England

JURGEN Klopp amepaza sauti kumsifia Fabinho kwa "kiwango bora" kwenye safu ya beki wa kati wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea, juzi Jumapili.

Huku Joe Gomez na Joel Matip wakiwa majeruhi, Fabinho alihamishiwa kwenye safu ya mlinzi wa kati kucheza pamoja na Virgil van Dijk na alionyesha kiwango cha kuvutia pale katika dimba la Stamford Bridge.

Mabao mawili ya Sadio Mane kipindi cha pili yaliinyanyua Liverpool katika ushindi wa pili mfululizo kwenye mwanzo wa Ligi Kuu England, huku straika huyo awali alidondoshwa na Andreas Christensen na kufanya mlinzi huyo kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

Klopp alimsifia Fabinho kwa kiwango chake, ingawa Liverpool ilihitaji Alisson kuokoa penalti ya Jorginho kuwafanya wamalize mchezo bila nyavu zao kutikiswa.

"Kama Sadio asingefunga mabao mawili, nafikiri Fab alipaswa kuwa nyota wa mchezo," alisema kocha huyo wa Liverpool akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilipenda kiwango chake, alicheza kwa ubora mzuri kabisa. Alitusaidia sana sisi kuzuia mipira langoni mwetu, ndio, alionyesha kiwango cha kuvutia sana."

# Gattuso: Ningependa Koulibaly abaki Napoli

**NAPLES,** Italia

KOCHA Mkuu wa Napoli, Gennaro Gattuso, anatambua kwamba, Kalidou Koulibaly anakaribia kuondoka kwa klabu hiyo ya Serie A, lakini atakuwa na furaha kama akimbakiza mlinzi huyo.

Koulibaly amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu England, Manchester City pamoja na Mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain, wakati Napoli wakiangalia uwezekano wa kutafuta fedha baada ya kumsajili, Victor Osimhen kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo.

Koulibaly mwenye umri wa miaka 29 alicheza wakati Napoli wakifungua msimu mpya wa Serie A kwa ushindi wa 2-0 dhidi ya Parma Jumapili na Gattuso alimsifia mlinzi huyo wa kati, ambaye pia anatajwa kuwaniwa na Manchester United.

"Sikuwa na shaka, yeye ni mmoja wa mabingwa wa dunia kwenye nafasi ya ulinzi wa kati," alisema Gattuso akiiambia Sky Sport.

"Mara zote amekuwa akiipa timu wakati mzuri. Nitasikitika kumpoteza kama mchezaji na kama mtu muungwana.

"Lakini unajua namba ni muhimu kwa klabu na wakati huu kitu fulani kinahitajika kuongeza namba ya wachezaji, lakini ningependa kumbakiza."

Osimhen aliichezea mechi yake ya kwanza Napoli, akitokea benchi wakati Dries Mertens na nahodha Lorenzo Insigne kila moja akifunga bao moja.



# Vidal atua Milan kujiunga Inter Milan

**MILAN,** Italia

ARTURO Vidal jana Jumatatu alitua jijini Milan, ili kukamilisha taratibu za usajili wa kujiunga na Inter Milan akitokea Barcelona.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile, ambaye awali alifanya kazi na Kocha Mkuu wa Inter, Antonio Conte kule Juventus, ametumia misimu miwili akicheza kule Camp Nou.

Vidal alicheza jumla ya mechi 43 kwa Barca msimu uliopita na ameonekana hayupo kwenye mipango ya kocha mpya wa Blaugrana hao, Ronald Koeman.

Nyota huyo ameondoka kwenye safu ya kiungo pamoja na Ivan Rakitic na Arthur.

Imeripotiwa kwamba, Inter italipa euro milioni moja kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye alikuwa kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba pale Barca.

Uhamisho huo ulitarajiwa kukamilishwa jana Jumatatu kabla ya nyota huyo kutangazwa rasmi kuwa ni mchezaji wa Inter.





# LAMPARD: BADO MSIIHUKUMU CHELSEA

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza ni mapema mno kuanza kutoa hukumu kama Chelsea itaweza kutoa changamoto kwa Liverpool katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Chelsea imetumia karibu pauni milioni 200 kujenga kikosi chake msimu huu, bado haikuwa kwenye kiwango bora mbele ya mabingwa hao watetezi hapo juzi usiku.

Huku Andreas Christensen akitolewa nje kwa kadi nyekundu kipindi cha kwanza, Sadio Mane alifunga mara mbili akitumia makosa ya golikipa, Kepa Arrizabalaga na Liverpool kuibuka na ushindi wa 2-0.

Timo Werner alipata penalti baada ya kufanyiwa faulo na Thiago Alcantara aliyekuwa anacheza mechi yake ya kwanza kwa Liverpool tangu atoke Bayern Munich, lakini Jorginho alishindwa kufunga kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge.

Hata hivyo, Lampard haamini kama matokeo hayo yanamaanisha hawezi kutoa changamoto ya ubingwa msimu huu.

"Natarajia sisi kuleta ushindani mkubwa kwa Liverpool. Tulishindana katika kila mchezo msimu uliopita," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa matukio ya Kepa ni makosa ya wazi. Kosa la wazi lililoigharimu timu na tukapata penalti lakini tukashindwa kufunga.

"Sidhani kama unaweza kutoa hukumu kwa sasa kwa hali jinsi mchezo ulivyokuwa kwa sababu tulijikuta tukicheza 10 dhidi ya 11 uwanjani."

# *Pirlo aeleza Ronaldo atakavyocheza Juventus*

**TURIN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Juventus, Andrea Pirlo anajua umuhimu wa kumpumzisha Cristiano Ronaldo na amesema mshambuliaji huyo ataamua ni mechi gani atakaa benchi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alifunga dakika za majeruhi wakati Juve ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Sampdoria pale kwenye dimba la Allianz, Jumapili wakati Pirlo akiongoza kwa mara ya kwanza klabu hiyo katika mechi ya kwanza ya msimu mpya.

Awali shuti lake liligonga mwamba, lakini baadaye alifunga katika dakika ya 88 akiunganisha pasi ya Emil Audero.

Huku mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or hivi karibuni alikuwa ameumia kidole kwenye mechi ya kimataifa, Pirlo anaonekana kufuatilia kwa karibu 'ufiti' wa nyota huyo.

"Tunafikiria kuhusu hilo na tumezungumza pamoja," amesema akiiambia Sky Sport Italia.

"Hajachoka kwa wakati huu kwa sababu ndio kwanza tumeanza msimu mpya. Lakini tutakapokuwa na mechi zisizo za muhimu sana tutajaribu kumpa mapumziko.

"Ni mchezaji mwenye akili na ambaye anajijua vizuri, hivyo anajua ni muda gani wa kupumzika. Wakati gani atacheza hilo litategemea na yeye mwenyewe."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# 'WACHEZAJI WAPYA WATAKIWA UNITED'

Ni ushauri uliotolewa na beki wa timu hiyo kama wanahitaji kufanya vizuri kwenye...

**MANCHESTER,** England

BEKI wa kushoto wa Manchester United, Luke Shaw (25), amesema klabu hiyo inatakiwa kusajili wachezaji wengine wapya ili kukiimarisha kikosi hicho cha Old Trafford au kujiweka kwenye nafasi ya kufanya vibaya kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

**United ilianza msimu mpya kwa kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Crystal Palace katika mechi iliyofanyika Jumamosi.**

Klabu hiyo imesajili mchezaji mmoja tu mpaka sasa, huku dirisha la usajili lilikaribia kufungwa wakati ndio kwanza Donny van de Beek akitua kwenye kikosi hicho akitokea Ajax, huku uhamisho wa winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho bado haujafanikiwa.

United pia ilikuwa katika mchakato wa kusaka beki wa kushoto, ili kuchukua mikoba ya Shaw lakini tayari imeshindwa kumnasa beki wa Real Madrid, Sergio Reguilon ambaye Jumamosi alitangazwa kujiunga na Tottenham kwa mkataba wa miaka mitano.

"Tuna kikosi kizuri sana, lakini binafsi nafikiri tunahitaji kusajili wachezaji wengine wapya ili kukiimarisha kikosi chetu," alisema Shaw.

"Yaani wakati ukiziangalia namna timu nyingine zilivyojenga vikosi vyao, na sisi tunatakiwa lazima tufanye kama hivyo ili kujiweka kwenye nafasi salama."

Wakati United ikishindwa kuwasajili nyota muhimu iliyokuwa inawahitaji kwenye dirisha hili la usajili, wapinzani wao wamefanikiwa kunasa nyota wenye viwango huku awali wakiwa imara pia.

Wiki iliyopita, Liverpool ilimsajili Thiago Alcantara akitokea Bayern Munich na Diogo Jota aliyekuwa Wolves, wakati Chelsea imetumia kiasi cha zaidi ya pauni milioni 200 kunasa wachezaji mbalimbali vijana wenye vipaji ambao wanatamba kwa sasa barani Ulaya.

Shaw alisema United inatakiwa kuhakikisha inaanza vyema kwa kujenga hamasa na kuondoka na ushindi kwenye mchezo wa Kombe la Ligi dhidi ya Luton Town utakaochezwa leo.

## ZISIKUPITE

### ALLI AIVURUGA SPURS

WACHEZAJI wa Tottenham wameshangazwa na uamuzi wa kumwacha nje kiungo wa England, Dele Alli, ambaye anahusishwa na mpango wa kujiunga na Paris St-Germain, kwenye mchezo dhidi ya Southampton ambao ulichezwa juzi na Spurs kuibuka na ushindi. ***(Mail)***

### RUDIGER NJIA PANDA

HATIMA ya beki wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger, ndani ya Chelsea iko mashakani baada ya nyota huyo kuachwa kwenye kikosi kilichopoteza mechi dhidi ya Liverpool juzi Jumapili, wakati mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 27 yuko fiti. ***(Mail)***

### MUSTAFI SOKONI

BEKI wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Shkodran Mustafi (28), anatajwa kuwindwa na klabu za Lazio na Napoli. The Gunners wamefungua milango ya kupokea ofa ya kumuuza nyota huyo. ***(Sun)***

### ARSENAL KUMTOA TORREIRA

ARSENAL inataka kumjumuisha kiungo wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Lucas Torreira (24), kama sehemu ya kufanikisha mchakato wa kumsajili kiungo Mghana Thomas Partey (27), kutoka Atletico Madrid. ***(El Gol, via Express)***

### MARLON ANUKIA FULHAM

FULHAM imewasilisha ofa ya kumsajili beki wa Sassuolo, Marlon (25), na kwa mujibu wa Mkurugenzi wa klabu hiyo ya Italia, Giovanni Carnevali, amesema mazungumzo kuhusiana na mchakato huo yanaendelea. ***(Sky Sports Italia, via Football Italia)***

### TELLES AIPOTEZEA UNITED

BEKI wa Timu ya Taifa ya Brazil, Alex Telles (27), anasisitiza anajiimarisha kuitumikia vyema Porto, licha ya kuhusishwa na mpango wa kujiunga na Manchester United. ***(Sport TV, via Metro)***

### CITY YAMGANDA KOUNDE

MANCHESTER City imeanza mazungumzo ya kusaidia ofa yake ya kumsajili beki Mfaransa, Jules Kounde, ambayo awali ilikataliwa na Sevilla. ***(Mirror)***

### BREWSTER AKARIBIA PALACE

CRYSTAL Palace inaongoza katika mbio za kumsajili straika wa Liverpool na Timu ya Taifa ya vijana ya England, Rhian Brewster (20), ambaye pia anawindwa na Sheffield United na West Brom. ***(Mail)***

### CHAMBERLAIN HAUZWI

MABOSI wa Liverpool wameweka wazi hawana mpango wowote wa kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Alex Oxlade-Chamberlain (27), ambaye anatakiwa na klabu ya Wolves. ***(Mirror)***

### LEICESTER, SPURS VITANI

LEICESTER City inajiandaa kuungana na Tottenham katika mbio za kuwania saini ya beki wa klabu ya Beijing Guoan na Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Kim Min-jae, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(90min)***

### MORRISON AITWA UHOLANZI

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Ravel Morrison (27), anajiandaa kujiunga na klabu ya ADO Den Haag ya Uholanzi baada ya kumaliza mkataba wa kuitumikia Sheffield United. ***(Omroep West, via Football Oranje)***

### VIDAL ATUA MILAN

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Chile, Arturo Vidal (33), alitarajiwa kufanya vipimo vya afya jana ili kukamilisha mchakato wa kujiunga na Inter Milan akitokea Barcelona. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

## Wanariadha wawili kushindana Poland

**Na Shufaa Lyimo**

WANARIADHA wawili wa hapa nchini, Gabriel Giay na Failuna Abdi wanaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya kwenda kuiwakilisha Tanzania kwenye mbio na nusu marathoni zitakazofanyika Oktoba, mwaka huu huko Poland, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Ombeni Zavalla, alisema maandalizi ya safari hiyo yako katika hatua za mwisho lakini amewaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuwaunga mkono wanariadha hao.

"Sasa hivi tunaandaa wachezaji wetu ambao watakwenda Poland kushiriki mashindano ya dunia, kiujumla wanaendelea vizuri na kinashosubiriwa ni tarehe ya mbio kutangazwa," alisema Zavalla.

Katibu huyo alisema mwanariadha ambaye atafanya vizuri na kufikia viwango vya juu, atapata tiketi ya kushiriki katika mashindano yajayo ya Olimpiki.

Mwanariadha Geay aliliambia gazeti hili anajiimarisha katika mazoezi anayofanya kwa sababu anahitaji kufikia malengo ya kurejea na medali.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi, kambi yetu iko Arusha, na hii imetokana na mazingira ya utulivu yaliyoko huku," mwanariadha huyo alisema.

## Ngumi wafurahi mipaka kufunguliwa

**Na Adam Nyangasa,** TUDARco

MABONDIA wanaoshiriki ngumi za kulipwa hapa nchini wanatarajiwa kuanza kusafiri kwenda katika mataifa mbalimbali kuwania mikanda ya ubingwa tofauti baada ya mipaka ya kutoka nje kuanza kufunguliwa, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makamu wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Aga Peter, alisema mataifa mbalimbali yameanza kuruhusu kuendelea kwa shughuli za michezo, hivyo wameanza kuwatafutia mabondia michezo.

Peter alisema kwa muda wote ambao mabondia walikuwa hapa nchini bila ya kupambana, waliendelea na programu mbalimbali za mazoezi ili kulinda viwango vyao.

"Tunashukuru serikali za nchi mbalimbali zimeanza kufungua milango, mapambano ya nje ya nchi yataanza kuchezwa, inamaanisha mabondia wetu watakwenda kupigana katika mapambano watakayoalikwa, ni uamuzi wa faraja kwetu," alisema kiongozi huyo.

Alisema waliandaa mashindano mbalimbali ya hapa nchini ili kuwaweka vyema mabondia wa hapa nchini na endapo watapata mialiko nje, hawatapata tabu ya kuwaweka tayari na michezo hiyo.

Alimtaja bondia Happy Daudi alipata nafasi ya kwenda Urusi kupigana ingawa mwakilishi huyo wa Tanzania alipoteza pambano hilo.

Hata hivyo aliwataka wadau na mashabiki wa mchezo huo waendelee kuunga mkono kwa kuwapatia udhamini kwa lengo la kuwaendeleza mabondia wa Tanzania.

# KAYUNI AZINDUA KITABU KUWAFUNDA WANASOKA

**Na Saada Akida**

WADAU wa soka nchini wametakiwa kumuunga mkono aliyekuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Sunday Kayuni, kwa kununua kitabu kiitwacho 'Kocha wa Soka' ili kufahamu mambo muhimu kuhusu mchezo huo hapa nchini.

**Kwa sasa Kayuni ni Mkufunzi wa Kimataifa anayetambuliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).**

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Nchini (BMT), Leodegar Tenga, alisema kitabu hicho kimeeleza mambo mbalimbali yanayohusu sifa ya kocha, falsafa pamoja na njia za kocha katika kuelimisha kwenye mchezo huo.

Tenga alisema kitabu hicho kitakuwa na maana hasa kitakaponunuliwa na kufanyiwa kazi mafunzo yaliyoandikwa.

"Mimi nitanunua 10, viwili nitapeleka baraza ili kuelimisha vijana wetu tunaowapa elimu mikoani, vitatu nitapeleka TFF kwa ajili ya kusoma kimoja apewe Rais, Katibu na Mkurugenzi wa Ufundi," alisema Tenga.

Alisema anatarajia shirikisho hilo litanunua vitabu na kuwapa makocha wao kwa ajili ya kupata elimu ambayo anaamini itasaidia katika kulipeleka mbele soka la Tanzania.


"Naamini kitabu hiki kitasaidia kuelimisha makocha na kupiga hatua kutoka hapo tulipo na kusonga mbele zaidi," alisema Tenga.

Aliongeza Kayuni ametimiza majukumu yake na watu wa michezo wengine wanatakiwa kujitokeza kuandika vitabu kwa ajili ya kunyanyua michezo hapa nchini.

Naye mwandishi wa kitabu hicho, Kayuni, alisema ilikuwa ni dhamira yake ya muda mrefu kuandika kitabu kwa lengo la kuelimisha makocha pamoja na wadau wote wa soka.

"Safari ya kuandika kitabu haikuwa nyepesi, nakumbuka 1988 nilianza kuandika na baadaye nikakipeleka baraza, kwa kunipongeza ila sikumbuki tena ile karatasi ya pongezi niliweka wapi, lakini hivi karibuni watu wakinifuata nakunihitaji niandike kitabu ikiwamo Tenga na wengine," Kayuni alisema.

Aliongeza amelazimika kufanya hivyo kwa sababu ya soka la sasa ni ajira na sio burudani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma na amelenga kwa makocha wapya kupata elimu kupitia andiko la kitabu hicho.




Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Leodegar Tenga (kulia), akimpongeza Mkufunzi wa Soka wa Kimataifa, Sunday Kayuni, baada ya kuzindua kitabu alichokiandika kiitwacho 'Kocha wa Soka' jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mgunda afunguka mastraika tatizo*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuambulia pointi moja, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema safu ya ushambuliaji imekuwa ni 'butu' na kusababisha wanakosa ushindi katika mechi zote tatu walizocheza za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mgunda alisema hayo baada ya kutoka suluhu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, jijini Tanga dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Kocha huyo alisema washambuliaji wake wanatengeneza nafasi nyingi, lakini suala la umaliziaji limekuwa ni tatizo.

"Ni kweli na lazima nikiri kuwa timu yangu upande wa ushambuliaji bado kuna matatizo, tunatengeneza nafasi nyingi, lakini hatuzitumii, lazima niseme kitu kimoja, mpira ni mchakato, ukileta maji ya moto kwenye kikombe hayo yanaitwa ni maji ya moto, lakini ukiweka majani ya chai na sukari hiyo inageuka inakuwa chai, kwa hiyo kidogo tutabadilisha hali hiyo na tutafika," alisema Mgunda.

Aliongeza anaendelea kurekebisha makosa yaliyojitokeza na katika mchezo wao unaofuata watapambana kusaka matokeo chanya.

"Unajua baada ya kupoteza mechi mbili, kutokana na uchanga wa wachezaji wangu, kama vile morali imepotea au wamepoteza kujiamini, sasa najaribu kuijenga tena ari ili wasitoke kwenye malengo, wasahau yaliyopita na waangalie mbele, naamini baada ya muda mfupi tu, vijana watarudi kwenye hali yao ya kawaida na tutafanya vizuri," Mgunda alisema.

Kabla ya kupata suluhu juzi, Coastal Union ilianza msimu mpya kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Namungo FC ugenini kwenye Uwanja wa Majaliwa halafu ikachapwa tena magoli 2-0 na Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam.

# Michezo

Jumanne Septemba 22, 2020

Nipashe




'Wachezaji wapya watakiwa Utd' UKURASA 22



Kiungo wa Simba, Larry Bwalya (kulia), akiwatoka wachezaji wa Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## KMC FC yazidi kuipoteza Yanga

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-1 ambao wameupata KMC FC dhidi ya Mwadui FC, umeendelea kuipa wakati mgumu Yanga ambayo ina pointi saba na mabao matatu ya kufungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Matokeo hayo, yameifanya KMC kufikisha pointi tisa na kurejea kileleni ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi tisa pia huku mabingwa watetezi, Simba wenye pointi saba wakiwa katika nafasi ya tatu, Dodoma JIJI FC ikifuatia na Yanga inashika nafasi ya tano kwenye msimamo.

Dakika 25 tu alizotumia uwanjani, zilitosha kumfanya straika mpya wa KMC, Reliants Lusajo, kuirudisha tena timu hiyo kileleni mwa Ligi Kuu Tanzania Bara, alipofunga mabao mawili na kuifanya timu yake ifikishe pointi tisa na kurejea kileleni.

Akitokea benchi, Lusajo, aliyesajiliwa na KMC akitokea Namungo FC ambapo msimu uliopita alimaliza ligi akiwa na mabao 11, alianza kufungua akaunti yake ya mabao msimu huu dakika ya 77 alipofunga bao la kusawazisha na kuirejesha timu yake mchezoni. Mwadui walitangulia kupata bao dakika ya dakika ya 11, kupitia kwa Issa Shaaban.

Dakika sita kabla ya mechi hiyo kumalizika, Lusajo alifunga bao la ushindi ambalo liliifanya KMC kupata ushindi wa tatu mfululizo katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

KMC iliengu liwa katika uongozi wa ligi na Yanga baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, ambayo nayo ilikuja kuenguliwa kileleni Jumapili jioni na Azam FC waliofunga Mbeya City bao 1-0 kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya.

Azam FC ambayo ilikuwa imeshinda mechi ya tatu mfululizo juzi, nayo iliongoza ligi kwa muda kabla ya KMC kurejea tena kileleni kwa kuwa na faida ya idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

# Sven: Burudani itaendelea

**Na Saada Akida**

### ●●● Awafunga 'midomo' walioibeza Simba, kocha huyo apendekeza Chama kupewa mkataba...

NI zaidi ya burudani! Mashabiki wa Simba walionekana kufurahi baada ya kumaliza mechi dhidi ya Biashara United huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, akisema kikosi chake kinatarajia kuendelea kutoa 'dozi' katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayofuata.

**Mabingwa hao watetezi juzi walipata ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Biashara United na kufikisha pointi saba, shukrani kwa wafungaji, Clatous Chama aliyefunga magoli mawili, Meddie Kagere na Chris Mugalu.**

Sven aliliambia gazeti hili kikosi chake 'kimetangaza vita' kwa mpinzani wao anayefuata na kusema wachezaji wake wamejipanga kuonyesha kiwango cha juu zaidi ya walichoonyesha katika mchezo uliopita.

Kocha huyo alisema wachezaji wake hasa wa kigeni wameonyesha kiwango kizuri na matumaini yake wataimarika zaidi na kuipa timu hiyo matokeo mazuri kwenye mchezo huo utakaochezwa Jumamosi usiku.

Aliongeza mbali na kucheza kwa kiwango kizuri na kuifunga Biashara United, kuna mapungufu madogo aliyaona na atafanyia kazi kabla ya kukutana na Gwambina ili wapate kile wanachokihitaji.

"Nimeridhishwa na kiwango kizuri walichokionyesha wachezaji wangu, natarajia hata mechi ijayo watacheza kiwango kizuri kama leo (juzi), au zaidi hasa ukizingatia tunacheza tena kwenye uwanja wa nyumbani," alisema Sven.

Alieleza malengo yao ni kuendelea kupata ushindi katika kila mechi na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutetea taji la Ligi Kuu Bara na kujiweka tayari na michuano ya kimataifa.

"Malengo yetu ni kuhakikisha tunatetea taji letu, tunahitaji kupambana ili kupata matokeo chanya katika kila mechi, hatutaidharau timu yoyote tutakayokutana nayo, kwa sababu ligi ni ngumu na imekuwa na ushindani mkubwa," Sven alisema.

"Mapendekezo yangu nahitaji kiungo wangu, Clatous Chama kuendelea kubaki katika kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao.

"Kama mkataba wake umebaki mwaka mmoja uongozi unatakiwa kumwongeza mapema, sipendi kuingilia uongozi ila kwa jinsi ya uwezo anaonyesha ndani ya kikosi hichi, bado timu inahitaji huduma yake," alisema Sven.

Alimtaja kiungo huyo kutoka Zambia ambaye alichagulia kuwa Mchezaji Bora wa msimu uliopita, amekuwa na mchango mkubwa ndani ya timu hiyo.

Naye Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, alisema hawezi kuwalaumu wachezaji wake kwa matokeo 'mabaya' waliyopata kwa sababu walizidiwa katika mechi hiyo.

"Tulikuja kutafuta suluhu, lakini Simba wakaziba mipango yetu hiyo, tumeadhibiwa bao hizo, hakuna tatizo ndani ya timu, wachezaji wamepambana kwa ajili ya kusaka matokeo ila mwisho wa siku tumepoteza kwa kuwa tulizidiwa mbinu," alisema Baraza.

Aliongeza kwa sasa wanakwenda kujipanga kurekebisha makosa waliyofanya ili kupata ushindi katika mechi inayofuata dhidi ya Ruvu Shooting.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >